# Kifurushi cha Zana za Majadiliano ya Vikundi Lengwa na Usaili

# Raundi ya Pili

Imeandaliwa na: Timu ya Utafiti wa MEWAKA nchini Tanzania iliyoongozwa na EdTech Hub

# Yaliyomo


Vikundi lengwa

- Mwongozo wa majadiliano ya kikundi lengwa cha walimu - raundi ya 2
  - Mahojiano mafupi na walimu wenye ulemavu au magonjwa sugu
  - Mwongozo wa majadiliano ya kikundi lengwa cha Mwezeshaji Rika, Mwalimu wa Taaluma na Mwalimu Mkuu

Usaili wa Wahabarishaji Muhimu Raundi ya pili

- Mwongozo wa mahojiano na mwakilishi wa serikali kuu
- Mwongozo wa usaili kwa Afisa Elimu Taaluma wa Mkoa (RAO)
- Mwongozo wa usaili kwa Afisa Elimu Maalumu wa Wilaya
- Mwongozo wa usaili kwa Afisa Elimu Kata (WEO)

Kiambatisho

- Hati ya ridhaa ya mdomo ya mshiriki wa utafiti

# Vikundi lengwa

## Mwongozo wa majadiliano ya kikundi lengwa cha walimu - raundi ya 2

**Lengo**: Vikundi lengwa vilivyo na majadiliano na mbinu shirikishi vinalenga kuangazia mienendo ya JzK/MEWAKA na kutoa fursa kwa sauti zilizotengwa ili kufahamisha utafiti mpana.

**Washiriki:** Hadi walimu 8 (wa kiume na wa kike) shuleni. Iwapo kuna zaidi ya walimu 8 shuleni,  washiriki hawatazidi 8 ndio wanaopaswa kushiriki kikundi lengwa.

Mwalimu Mkuu, Mwezeshaji Rika na Mwalimu wa Taaluma au Mratibu Elimu Kata wanaoshiriki katika mahojiano hawapaswi kuwa sehemu ya kikundi lengwa hiki cha mwalimu. Ikiwa kuna walimu wenye ulemavu shuleni, tungependa washiriki katika kikundi lengwa.

### Mwongozo kwa mtafiti:

*Tafadhali soma miongozo ya mtafiti kwa utafiti ulio katika lugha ya Kiingereza.*

**Maandalizi kabla ya kuanza majadiliano na kikundi lengwa kwa raundi ya pili:**

1) Hakikisha umejiandaa kwa ajili ya kuwasilisha matokeo na mapendekezo ya raundi ya kwanza kwa haraka na uhakika. (Kwa wastani, usitumie zaidi ya dakika tano kuwasilisha matokeo au mapendekezo).

2) Andaa zana zifuatazo kwa idadi inayolingana na idadi ya walimu watakaoshiriki katika kikundi lengwa:
    - kalamu nyeusi kwa kila mwalimu wa kike
    - kalmau ya buluu ya nyekundu kwa kila mwalimu wa kiume
    - au kalamu yenye rangi tofauti ili kutofautisha jinsi (kama utatumia rangi mbalimbali hakikisha unaandika kumbukumbu, k.m. “nyeusi = -ke; rangi nyingine = -me” au “rangi nyeusi, buluu, kijani = -ke, rangi nyekundu au njano = -me”)
    - maka peni nyeusi 2-3 (kwa vikundi vya wanawake) na nyekundu 2-3 (kwa vikundi vya wanaume)
    - kamera au simu janja kwa ajili ya kupiga picha za matokeo ya shughuli
    - kinasa sauti
    - manila
    - ubao, kuta safi au meza safi kwa ajili ya kuweka kadi na ‘stiicky notes’
    - ‘sticky notes’ isiyopungua 5 kwa kila mwalimu

3) Machapisho yenye maandishi makubwa ya matokeo na mpendekezo ya

raundi ya kwanza ya utafiti

4) Nakala za matokeo na mapendekezo ya raundi ya kwanza ya utafiti, kwa ajili ya kuwapitia kila mwalimu mkuu na afisa wa elimu atakayeshiriki.
    a) kwa ajili ya shughuli ya kupanga mapendekezo (Katika Kundi Lengwa la walimu na usaili na maafisa wa elimu): chapisha kadi ndogo ndogo, kila kadi ikiwa na pendekezo moja kutoka raundi ya kwanza.
    b) kalamu ya 'whiteboard' au penseli kwa ajili ya kuandika namba kwenye kila kadi ikishapangwa na washiriki.

5) Andaa zana zifuatazo kwa ajili ya shughuli ya "mabadilko katika ufundishaji":
    - "sticky notes" tatu kwa kila mwalimu
    - ukuta au meza safi kwa ajili ya kupanga "sticky notes"

## Utangulizi na idhini

Habari, jina langu ni ________________________. Ningependa kukuomba ruhusa ya kushiriki katika programu ya utafiti ambayo inalenga kuchunguza _____________________________________. Utafiti huu unafadhiliwa na ______________________________________________________________

Majadiliano haya ya kikundi lengwa yamegawanyika katika sehemu tatu

- Kwanza, tungependa kuwasilisha matokeo muhimu ya raundi ya kwanza ya utafiti na kujadili haya nanyi.
- Kisha, tungependa kujadili na kuweka kipaumbele kwa mapendekezo tuliyounda kutoka kwa matokeo hayo.
- Katika sehemu ya tatu, tutafanya shughuli ili kupata maoni yenu kuhusu mabadiliko yoyote katika ufundishaji wako,

Lengo letu ni kuelewa ni mambo gani yanayoathiri maendeleo ya kitaaluma ya walimu, na ni kwa njia zipi MEWAKA inaweza kuwa na ubora na usawa zaidi, ili kukidhi mahitaji ya walimu wote. Matokeo yatatumiwa kuimarisha programu ya kitaifa ya MEWAKA.

Majadiliano ya kikundi lengwa yatachukua takribani saa 1 u (saa 1 na dakika 15)

Ni chaguo (hiari) lako kushiriki au kutoshiriki. Ukiamua kushiriki, unaweza kukataa kujibu maswali yoyote ambayo hautayafurahia, na unaruhusiwa kujiondoa wakati wowote. Ukichagua kushiriki, taarifa zako binafsi utazoniambia hazitashirikiwa na mwalimu mkuu au mtu mwingine yeyote katika shule na haitathiri jukumu lako kama mwalimu. Tutarekodi mazungumzo haya kwa kinasa sauti na picha ili tujumuishi majibu yako katika ripoti za utafiti, lakini hatutakutaja kwa jina au kushirikisha maelezo yako binafsi kwa mtu yeyote nje ya timu yetu.

Taarifa zote unazotoa zitahifadhiwa kwa usalama, na hazitaonekana na mtu yeyote aliye nje ya timu ya utafiti, ambayo ni ya washiriki wa timu ya utafiti pekee.

Hata hivyo, ikiwa ninaamini kwamba yeyote kati yenu au mtoto anaweza kuwa katika hatari, ni wajibu wangu kuripoti hili kwa mtu husika.

Taarifa/data isiyotambulika inaweza kuonekana katika hazina wazi, machapisho na mawasilisho. Itatumika tu kwa madhumuni ya utafiti na maendeleo ya kitaaluma ya walimu, ikijumuisha tafiti zijazo na uchanganuzi wa taarifa/data.

1. Je, kuna maswali yoyote kabla hatujaanza?
2. Je, unakubali kushiriki katika majadiliano/utafiti/ uchunguzi huu wa kikundi? [Hakikisha kila mshiriki ana nafasi ya kujibu hili]
   a. Ndio
   a. Hapana (waambie wako huru kwenda)

## Usimamizi wa kikundi lengwa

Sitaki kuwaweka kwa muda mrefu, hivyo nitakuwa nikisimamia matumizi ya muda kwa uangalifu. Ninataka kukufahamisha kwamba huenda nikahitaji kukusogeza kwenye mada inayofuata! Tafadhali usikwazike ikitokea hivyo."

Wakati wa majadiliano, tafadhali kumbuka kanuni zifuatazo:

- Jisikie huru kutoa maoni na uzoefu tofauti wakati wa majadiliano
- Tafadhali soma kwa sauti unachoandika (hii ni ili yeyote aliye na ulemavu wa kuona aweze kusikia mchango wa wengine au kwa madhumuni ya kurekodi sauti).
- Tafadhali usijadili mazungumzo au shughuli za kikundi lengwa na watu wengine nje ya kikundi hiki.
- Heshimu michango ya washiriki wote na uwe mwangalifu ikiwa unatawala mazungumzo au unasitasita kuwasilisha maoni yako. Sote tusaidie kuhakikisha mchango wa usawa wa walimu wote.

## Taarifa za kurekodi

*Ijazwe na mtafiti kabla ya kuanza FGD*

| | |
|---|---|
| **Jina la mtafiti** | |
| **Tarehe ya FGD** | |
| **Eneo shule ilipo** | |
| **Jina la Shule** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 1** | |

| | |
|---|---|
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 2** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 3** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 4** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 5** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |

| Taarifa za mshiriki wa 6 | |
|---|---|
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 7** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 8** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |

### Maelezo kuhusu walimu wenye ulemavu:

Iwapo mwalimu yeyote katika kikundi lengwa ana ulemavu unaojulikana (kwa kutumia data ya uchunguzi wa walimu ikiwa inapatikana kabla ya kipindi), tafadhali onyesha hapa ni nambari gani ya mshiriki na aina ya ulemavu [usiulize mbele ya kikundi]:

Orodhesha mabadiliko yoyote yaliyofanywa na walimu, mwezeshaji rika au watafiti ili kujumuisha walimu wenye ulemavu au mahitaji mengine katika shughuli:

### Vidokezo vya kuanzisha na kujadili itifaki:

- Panga walimu katika mduara au nusuduara
- Wape walimu namba kulingana na nafasi zao za kukaa
- Pitisha kinasa sauti kama maikrofoni ili kurekodi sauti kwa uwazi.

- Endelea kuwapa walimu nafasi ya kutoa maoni, kuongeza, kukanusha, kuhoji majibu ya kila mmoja wao. Hakikisha kuna uchangamani miongoni mwa walimu.
- Hakikisha walimu wote wana nafasi ya kuzungumza, elekeza maswali kwa watu mahususi, ruhusu jibu 1 au 2 kwa kila kipengele.

## Sehemu ya 1: Matokeo ya Utafiti ya Raundi ya I

[dakika 20]

*[Angalizo kwa watafiti: Endelea kurekodi hadi hatua ya 4]*

**Hatua ya 1: Bandika** matokeo ya utafiti ya raundi ya kwanza ya utafiti ili washiriki wote wa kikundi lengwa waweze kuyaona. *[Angalizo: Mtafiti saidizi abandike wakati 'lead interviewer' anachukua taarifa na idhini za washiriki].*

> *1b: Eleza kwamba matokeo na mapendekezo yamewasilishwa ngazi ya kitaifa (WIZARA), na tunawasilisha kwa ngazi za kata, wilaya na mkoa pamoja na shuleni.*

**Hatua ya 2: Soma matokeo makuu** ya utafiti huku washiriki wakitazama matokeo yaliyochapishwa kwenye mabango madogo.

*[Angalizo: Matokeo ya utafiti wetu yamejumuishwa hapa kama mfano - yanapaswa kubadilishwa yawe matokeo ya utafiti wako]*

1. **Walimu wenye ulemavu:** Kati ya walimu 125 kutoka (MKOA), walimu 14 waliripoti kuwa na ulemavu uliochunguzwa kitalaamu, na 12 walikuwa na magonjwa sugu kama vile kisukari au pumu. Ni muhimu kutambua kwamba idadi ya walimu wenye ulemavu waliobainisha wenyewe ilikuwa kubwa zaidi kuliko ile iliyotolewa na walimu wakuu. Walimu wenye ulemavu waliripoti kwamba vishikwambi, moduli kutoka katika mfumo wa ujifunzaji (LMS), na programu hazina msaada wa kutosha kwa wenzao wenye uoni hafifu.
2. **Mabadiliko:** Shule zilizo na walimu wenye ulemavu zilitumia mikakati mbalimbali ili kuongeza usawa katika ushiriki katika jumuiya za ujifunzaji, ikiwa ni pamoja na kutumia mbinu za ushirikiano na uchangamani (kama vile mijadala), kusaidia walimu wenye ulemavu kushiriki, na kuhakikisha mawasiliano yanakuwa wazi. Hakuna marekebisho ya matini za ujifunzaji zilizobainishwa. Pia wadau walibaini kutokuwepo kwa mwongozo wa namna ya kutoa msaada kwa walimu wenye ulemavu.
3. **Ushiriki wenye usawa wa kijinsia katika JzK:** Ni asilimia 38 tu ya wawezeshaji rika walikuwa wanawake. Walimu wa kiume na wa kike hushiriki kwa usawa katika vikao vingi (8 kati ya 12) vya JzK. Aidha, katika shule 4 kati ya 12, kulikuwa na ukosefu wa ushiriki sawa. Vizuizi vinavyohusiana na jinsia vilivyobainishwa ni pamoja na umakini mdogo wa wawezeshaji rika katika kuhakikisha walimu wote wanashiriki kwa usawa. Katika JzK zilizokosa ushiriki kwa usawa, mara nyingi ushiriki wa walimu wa kike ulikuwa mdogo hasa katika vipindi vinavyohusiana na teknolojia.

4. **Uwezo wa kukidhi mahitaji ya walimu:** Walimu wanakidhi mahitaji yao kupitia njia zifuatazo: i) kuweka vipaumbele vya JzK, ii) kutumia data za simu za mkononi katika MEWAKA, na iii) kutoa msaada wa kiteknolojia kwa wenzao. Baadhi ya shule zilitoa vifurushi vya intaneti au chakula kwa walimu. Pia Mthibiti Ubora wa Wilaya moja alianzisha kundi la WhatsApp la walimu. Hata hivyo, karibu washiriki wote waliona kuwa walimu wana nafasi ndogo ya kufanya maamuzi, na shule kadhaa zilihisi kuwa hazikuwa na msaada ikiwa mahitaji ya kiufundishaji ya walimu yasingeweza kutatuliwa ndani ya shule.

5. **Taratibu zinazoruhusu mrejesho ili kukidhi mahitaji ya walimu:** Taratibu zimewekwa ili kubadilisha shughuli za JzK ili kukidhi mahitaji ya walimu ndani ya shule na kata, ikiwa ni pamoja na kushughulikia changamoto na kueneza ubunifu. Hata hivyo, mkoa wa (MKOA) pekee ndiyo uliokuwa na utaratibu wa kutoa mrejesho na kuufanyia kazi kikamilifu kuanzia ngazi ya shule, kata, Kituo cha Walimu (TRC) na wilaya.

6. **Mahitaji ya walimu ambayo hayawezi kutatuliwa katika ngazi ya shule kwa kiasi kikubwa yanabaki bila msaada.** Kwa mfano, mahitaji ya miundombinu ya mawasiliano, pamoja na ukosefu wa vifaa, ujuzi mdogo wa kidijitali wa walimu, upatikanaji wa vifaa vya teknolojia saidizi kwa walimu wenye ulemavu, gharama za data, kukosekana kwa mtandao, na matatizo ya upatikanaji na matumizi ya LMS.

**Hatua ya 3: Uliza kikundi:** Je, kuna maswali yoyote ya ufafanuzi kabla hatujaingia kwenye shughuli? [*Subiri na kujibu maswali yoyote]*. Sasa tutaifanya shughuli ili kukusanya maoni na maelezo yenu kuhusu matokeo tuliyowashirikisha.

*[Angalizo kwa watafiti: **Hakikisha maswali ni yale yanayofafanua matokeo yaliyowasilishwa**. Ikiwa washiriki wanataka kutoa mawazo/maoni yao, eleza kwamba watapata fursa ya kufanya hivyo katika shughuli inayofuata.]*

**Hatua ya 4: *Sitisha kurekodi.* *Wagawe walimu katika vikundi vya walimu wa jinsia moja*** *(Ikiwa, siku hiyo, kuna mwalimu mmoja tu wa kiume au wa kike, fanya FGD ya jinsia mchanganyiko (mixed gender) na ugawanye nyenzo hizi kwa kila kikundi*

- Bango kitita
- Vidakuzi (~ 10 kwa kila kundi)
- Kalamu - Hakikisha vikundi vya walimu **wa kike vinapata kalamu nyeusi** , na vikundi vya walimu **wa kiume vinapata kalamu za buluu au nyekundu.**

**Kama walimu wamegawanika kwenye vikundi vya jinsia moja,** hakikisha kikundi kimoja kinatoka na kukaa katika sehemu nyingine, mtafiti mmoja akiwaongoza kwa hatua ya 5 hadi hatua ya 9. Endelea kurekodi shughuli nzima (kwa maana hiyo mtafiti ambaye anatoka na kikundi kimoja atumie kishikwambi (tablet) yake kurekodi mpaka watakaporudi kwenye kundi zima (Hatua ya 9).

**Hatua ya 5: Waambie walimu:** "Nitawauliza maswali kadhaa. Kwa kila swali, ningependa kila mmoja wenu aandike jibu lake mwenyewe kwenye kidakuzi.

Tafadhali andika jibu lako binafsi kwenye kidakuzi tofauti kwa kila swali- yaani andika jibu moja tu katika kila kidakuzi”

> **Swali la 1:** Ni mawazo gani ya kwanza yalikujia baada ya kusikia matokeo haya? [Subiri ili kuwapa walimu muda wa kuandika jibu lao kwenye kidakuzi]
>
> **Swali la 2:** Ni matokeo gani yaligusa zaidi moyo wako? Kwa nini? [Subiri ili kuwapa walimu muda wa kuandika jibu lao kwenye kidakuzi]

**Hatua ya 6: Eleza:** “Sasa bandika vidakuzi vyako kwenye bango kitita, ”

> **[ANZA KUREKODI]**
>
> **6b: Mshiriki mmoja asome kwa sauti majibu yaliyobandikwa kisha wajadiliane** [hatua hii isizidi dakika 5]
>
> [*note to researchers: include the responses as read aloud in the transcript]*

**Hatua ya 7: Gawa** bango kitita mpya na kalamu rashasha kwa kila kundi (nyeusi kwa wanawake, bluu/nyekundu kwa wanaume) **na waambie wote watulie na kusikiliza maelekezo yanayofuata.**

**Hatua ya 8: Eleza:** Je, kuna vikundi vilivyojadili matokeo yanayohusiana na jinsia? Nitauliza maswali machache kuhusu tokeo hilo. Tafadhali jadilieni na andikeni majibu yenu ya maswali haya kwenye bango kitita mpya kwa pamoja kama kundi ukitumia kalamu rashasha.”

> **Swali la 3a:** Je, mlishangaa kusikia kwamba wanawake hushiriki kwa kiasi kidogo katika vipindi ya JzK vinayohusiana na teknolojia? *[Angalizo: Kwenye bango kitita, waandike “tulishangaa” au “hatukushangaa” au “baadhi yetu tulishangaa”]*
>
> **Swali la 3b:** Kwa maoni yenu, kwa nini unadhani hali hii inatokea? *[Waorodheshe majibu yao]*
>
> **Swali la 3c:** Mnapendekeza hatua gani zichukuliwe ili kushughulikia hali hii? *[Waorodheshe mapendekezo yao/ushauri wao]*
>
> *[KUMBUKA: Majadiliano ya vikundi vidogo hayahitaji kunakiliwa, lakini ni muhimu kuweka vinasa sauti vikiwa vimewashwa ikiwa tutataka kufuatilia chochote ambacho majadiliano yataibua kwenye rekodi wakati wa uchambuzi]*

**Hatua ya 9: Baada ya makundi kumaliza kuandika kwenye bango kitita, warejee kwenye kundi moja . Wape nafasi kutazama bango kitita za vikundi vingine** *[a quick gallery walk -only 1 or 2 minutes - flip charts can be on tables or on the wall]*

**Hatua ya 10: Anza kurekodi tena kisha Uliza washiriki:** Sasa mmeona mawazo ya vikundi vingine. Je, kuna jambo lolote lingine mngependa libainishwe au kujadiliwa, iwe kutokana na majadiliano katika kundi lenu au vile mlivyoona kwenye bango kitita za vikundi vingine?

***Angalizo: Bandika kidakuzi chenye tarehe, shule, na nambari ya kundi (1, 2, 3) kwenye bango kitita za kila kundi kisha piga picha za kila bango kitita*** *(kutoka kwa vikundi vyote). Hifadhi picha hizo na hakikisha zinajumuishwa katika transcript ya kikundi lengwa**.** [If it is not convenient at this moment, be sure to do this at the end of the FGD. ]*

## Sehemu ya II. Kuweka Kipaumbele Mapendekezo ya Raundi ya 1 ya Utafiti

[dakika 20]

***[Sitisha kurekodi hadi Hatua ya 5]***

**Hatua ya 1: Bandika mapendekezo (large print)** mahali ambapo washiriki wote wanaweza kuyaona.

**Hatua ya 2: Eleza** kwamba kulikuwa na mapendekezo kadhaa kulingana na matokeo ya raundi ya kwanza **na zungumzia** kwa kifupi (wasilisha) mapendekezo haya.

> ***Baada ya kuwasilisha , uliza:*** Je, kuna maswali yoyote ya ufafanuzi wa mapendekezo haya?

**Mapendekezo**

*[Angalizo: Mapendekezo ya utafiti wetu yamejumuishwa hapa kama mfano - yanapaswa kubadilishwa yawe mapendekezo ya utafiti wako]*

**Taratibu Saidizi:**

1. Kuongeza ufahamu wa moduli za JzK: Hakikisha kwamba wadau wote (wakuu wa shule, wawezeshaji rika, WEOs, na DSQAOs, n.k.) wanaelewa asili ya muktadha wa MEWAKA na wana vifaa vya kutosha kusaidia na kutekeleza MEWAKA katika ngazi ya shule.
2. Kukuza na kutekeleza taratibu za kutoa mrejesho wa mahitaji ya walimu: Kushughulikia mahitaji ya walimu ambayo hayajatatuliwa katika ngazi ya shule na kuwawezesha kusambaza maarifa na kuiga ubunifu katika MEWAKA kati ya shule moja na nyingine. Hii inaweza kujumuisha:
    a. Kuwa na mifumo bora ya kusaidia shule/walimu wanapokutana na changamoto katika utekelezaji wa JzK/MEWAKA.
    b. Kuhakikisha usambazaji endelevu wa bunifu zenye ufanisi katika ya shule zote.

**Miundombinu na Teknolojia:**

3. Kuongeza upatikanaji wa moduli za JZK kwa shule zenye mtandao za intaneti ambazo ni hafifu kwa kutathmini na kujaribisha utekelezaji wa upatikanaji wa moduli bila kutumia mtandao (offline) na/au kutafuta upatikanaji wa bure wa LMS kwa walimu kupitia watoa huduma wa mitandao ya simu.
4. Kutekeleza upatikanaji wa umeme wa jua kwa shule zisizo na umeme ili kuwawezesha walimu kuzifikia LMS na moduli za JzK.
5. Kukuza tabia za kuazimana vifaa vya teknolojia baina ya walimu katika ngazi ya shule.
6. Kuchambua changamoto zinazojitokeza katika matumizi ya vishikwambi vilivyotolewa hivi karibuni kwa walimu katika muktadha mbalimbali wa shule.

**Usawa: Walimu wenye Ulemavu**

7. Kupanua dhana na ubainishaji wa ulemavu ili kuhakikisha kwamba takwimu za elimu zinakusanywa kwa usahihi. Hii ikijumuisha taarifa za walimu wenye ulemavu wa kuona, kusikia, na kutembea, na pia kuhusisha ulemavu wa aina nyingine, kwa mfano ulemavu wa akili.
8. Kurasimisha utoaji wa msaada kwa walimu wenye ulemavu ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za MEWAKA kwa kuandaa mwongozo toshelevu na jumuishi utakaoshughulikia mahitaji yao na changamoto zao maalumu. Pia kutoa teknolojia saidizi kama za usomaji wa skrini, kuandaa ruzuku za walemavu ili kusaidia usafiri, na kuanzisha mitandao ya walimu wenye ulemavu kati ya shule na shule.

**Usawa: Jinsia**

9. Kuweka mikakati ya kuongeza ushiriki wa walimu wa kike katika vikao na shughuli za JzK. Hii inaweza kujumuisha:
    a. Kuteua Maafisa wa TEHAMA wa Wilaya na mabingwa wa TEHAMA wa shule kuwa na jukumu la kusaidia walimu wenye ujuzi mdogo wa kidijitali kutumia LMS na vishikwambi vilivyotolewa na serikali.
    b. Kuwepo mwongozo na ufuatiliaji ili kuhakikisha idadi ya wawezeshaji rika wa kike na wa kiume inalingana.
    c. Kuandaa warsha na mafunzo maalum ili kuwasilisha na kushughulikia matokeo kuhusu ushiriki wa jinsia na utofauti uliopo.

**Hatua ya 3: Waombe walimu warejee** kwenye vikundi vya jinsia moja. Wape kila kundi seti ya kadi za mapendekezo.

**Hatua ya 4: Waombe walimu kupanga** mapendekezo kutokana na umuhimu au kipaumbele yake - yapi ni muhimu zaidi na yanapaswa kushughulikiwa kwanza, ili kuendelea kuboresha MEWAKA.

- **Wafanye kwa pamoja kama kundi, wakijadiliana ili kufikia makubaliano kuhusu mpangilio.**
- Waambie waweke kadi kwa mpangilio, kuanzia **1 kama kipaumbele cha juu au muhimu zaidi hadi 9 kama kipaumbele cha chini.**

**Hatua ya 5: Anza tena kurekodi** baada ya kuwa wamepanga kadi kwa mpangilio wa kipaumbele**. Uliza maswali haya,** na hakikisha unapata jibu kutoka kwa kila kundi:

> **Swali la 4a:** Ni kipaumbele gani cha kwanza kwenu na kwa nini hilo ndio pendekezo muhimu zaidi?
>
> **Swali la 4b:** Je, kulikuwa na mapendekezo yoyote ambayo mlitofautiana kwenye kikundi, yaani, pendekezo ambalo mtu mmoja au zaidi walidhani linapaswa kuwa na kipaumbele cha juu au cha chini? Ikiwa ndiyo, tafadhali elezea kwa ufupi maoni tofauti kuhusu pendekezo hilo (au mapendekezo hayo, ikiwa ni zaidi ya moja)
>
> **Swali la 4c:** Je, kuna mapendekezo mengine yoyote mngetaka kuongeza ili kuboresha JzK au MEWAKA?

***Angalizo: Weka kidakuzi*** *chenye tarehe na namba ya shule kwa kila mpangilio wa kadi za kundi,* ***kisha piga picha za kadi za mapendekezo zilizopangwa.*** *Hifadhi picha hiyo na hakikisha inaingizwa katika maandiko ya kikundi lengwa.* ***[****If it is not convenient at this moment, be sure to do this at the end of the FGD. ]*

## Sehemu ya III. Mabadiliko ya Utendaji wa Walimu

[Dakika 10]

*[Angalizo: Shughuli hii mtafanya kwa pamoja, sio kwenye vikundi vidogo. kwa maana hiyo, utatoa maelekezo kwa washiriki wote, kisha kila mmoja ataandika mifano yake kwenye kidakuzi chake, halafu mtazipanga ("clustering") kwa pamoja ili itoke bango kitita moja tu kwa FGD]*

**Hatua ya 1: Eleza** kwamba katika shughuli hii ya 3, tungependa kujua ni mabadiliko gani walimu wamefanya kutokana na kushiriki katika JzK/MEWAKA.

**Hatua ya 2: Mpe kila mwalimu kidakuzi.**

- Hakikisha wanaume wanatumia kalamu ya bluu (au nyekundu) na wanawake wanatumia kalamu nyeusi.

**Hatua ya 3: Uliza:** Je, kumekuwa na mabadiliko yoyote katika ufundishaji wako kutokana kushiriki JzK au MEWAKA

**Ikiwa hakuna mabadiliko, nenda shughuli inayofuata.**

**Ikiwa walimu wanasema ndiyo,** kumekuwa na mabadiliko, waelekeze kuandika mfano mmoja wa mabadiliko muhimu zaidi katika kazi yao kwenye kidakuzi. Kila mtu aandike mfano wake. Kama ana mifano mengi, achague moja tu ambayo anaona ni muhimu zaidi.

- Eleza kwamba mifano inapaswa kuwa mahususi iwezekanavyo. Toa mifano kama:
  - "Ninazungumza na wenzangu kuhusu changamoto za kielimu zaidi kuliko ilivyokuwa awali; na niliweza kupata mawazo kutoka kwa X[fulani] jinsi ya kuwafanya wanafunzi wapweke wazungumze zaidi."
  - "Ninabadilishana vifaa na mawazo na wenzangu wakati wa mapumziko, kwa mfano, nilishiriki XXX."
  - "Sasa ninatumia kazi za kundi katika madarasa yangu ya hisabati angalau mara moja kwa wiki."
  - "Kutokana na moduli ya Elimu Jumuishi, nilitambua mahitaji maalum ya wanafunzi wangu mwanzoni mwa mwaka huu, na ninatoa umakini wa ziada kwa wale wanaohitaji muda zaidi kujifunza."

*[TIP: zunguka wakati walimu wanaandika. Ukiona wameandika juu juu, waulize maswali ili waongeze maelezo kwenye kidakuzi. Kwa mfano, kama ameandika "Sasa ninatumia zana" - Je, zana gani? zimetengenezwa na nini ? Nani a(wa)lizitengeneza/zimetokea wapi ?l? Anatumia kufundisha somo gani?]*

**Hatua ya 4: Kuunganisha majibu**

- Waombe walimu wote kuweka kadi zao kwenye meza au ukuta, kisha, kama kundi, waunganishe majibu.
  - Unganisha mabadiliko ya mtu mmoja na yale ya wengine kwa kuunganisha mifano inayofanana

***NB: Ongeza kidakuzi chenye tarehe na namba ya shule; kisha piga picha za vidakuzi vilivyopangwa.*** *Hifadhi picha hiyo na hakikisha inaingizwa katika maandiko ya FGD. [If it is not convenient at this moment, be sure to do this at the end of the FGD].*

## Mwisho wa mahojiano

Asanteni nyote kwa muda wenu na kwa kujibu maswali yangu yote - hilo lilikuwa swali langu la mwisho kwenu.

1. Je, kuna kitu kingine chochote ambacho ungependa kuniambia kuhusu wewe au MEWAKA/JzK ambacho hatujakijadili?
2. Je, kuna yeyote kati yenu ana swali lolote kwangu kabla hatujamaliza?
3. [Ikiwa mahojiano ya kundi dogo hayajafanyika bado] Kumbuka kwamba kila mtu anayehisi ana ulemavu au ugonjwa sugu anakaribishwa kujiunga na mahojiano maalum ya kundi dogo. Mahojiano haya yatatoa nafasi salama na ya msaada kwa wewe kujadili mahitaji yako maalum na kuwasilisha maoni yako. [Waambie mtafanya mahojiano haya wapi na saa ngapi[

**Maoni - kisanduku hapa chini kitajazwa na watafiti baada ya mahojiano ya kikundi lengwa:**

| |
|---|
| *Tafadhali andika tafakuri au madokezo yoyote ambayo unafikiri ni muhimu kwa timu ya utafiti au washirika wengine kuyafahamu. Tafadhali onesha jinsi ushiriki ulivyokuwa wa usawa.* |

# Mahojiano mafupi na walimu wenye ulemavu au magonjwa sugu

**Lengo:** Kuchunguza kwa kina masuala yanayowakumba walimu wenye ulemavu, katika mazingira salama. Kuwashirikisha matokeo muhimu na mapendekezo ya raundi ya kwanza ya ukusanyaji wa data na kukusanya maoni.

**Maelekezo**

**MAANDALIZI YA AWALI**:

- Mara unapofika shuleni siku ya kwanza, au unapowasiliana nao mapema, muombe mkuu wa shule kuwakaribisha walimu wanaojiona kuwa na ulemavu au ugonjwa sugu unaoathiri ushiriki wao katika MEWAKA kujiandikisha kwa ajili ya mahojiano mafupi katika kundi. (Tunataka kuepuka kuwatambua hadharani wale wenye ulemavu au magonjwa sugu, baadhi ya ambayo yanaweza kuwa ya siri.)
- **Omba mkuu wa shule aeleze sababu ya kuandaa mahojiano haya** – kutoa nafasi salama na ya msaada kwa walimu wenye ulemavu au magonjwa sugu kujadili mahitaji yao na kuwasilisha maoni yao bila uwepo wa walimu wengine, na kuhamasisha (bila kulazimisha!) walimu kuchukua fursa hii.
- Ikiwa walimu wenye ulemavu waliowekwa wazi hawatakuja mbele, unaweza kuzungumza nao kwa faragha ili kuangalia kama wangeweza kujiunga.
- Mwishoni mwa mahojiano ya kundi lengwa cha walimu, unaweza pia kuwaarifu kuhusu mwaliko, lakini ushiriki si wa lazima hivyo tunahitaji kuheshimu mapendeleo yao.

**IDADI YA WASHIRIKI:**

- Ikiwa kuna mwalimu mmoja tu mwenye ulemavu/ugonjwa sugu, anaweza kushiriki katika mahojiano kama yuko tayari. Ikiwa wapo wengi, utaendesha mahojiano kama FGD.

**IDHINI**

- Kama mmeshafanya FGD ya walimu na walimu hao hao walihudhuria, **w**atakuwa tayari wamekubali kushiriki katika kikundi lengwa. Kwa hiyo la kusema ni: “Ulikubali kushiriki na kurekodiwa wakati wa kikundi lengwa – je, uko tayari kwa idhini ile ile kuendelea na mahojiano haya pia?”

- Kama mahojiano haya yanafanyika **kabla** ya kikundi lengwa cha walimu au baadhi ya walimu hawakuhudhuria kikundi lengwa tumia “Hati ya ridhaa ya mdomo ya mshiriki wa utafiti” kutoa utangulizi na kupata idhini kabla ya kuanza mahojiano.
- Angalizo: Mahojiano yanatarajiwa kuchukua kati yaHati ya ridhaa ya mdomo ya mshiriki wa utafiti dakika 30 - 45

**Taarifa za kurekodi**

*Kukamilishwa na mtafiti kabla ya kuanza mahojiano. [Ikiwa tayari una maelezo baadhi kwenye fomu ya kikundi lengwa cha walimu, usiulize tena bali nakili maelezo hayo mwenyewe baadaye. Rekodi majina yao na ulemavu/ugonjwa wao kwa sasa. Ikiwa mwalimu yeyote hakuwa na uwepo kwenye kikundi lengwa, nukuu maelezo yao yote.]*

| | |
|---|---|
| **Jina la mtafiti** | |
| **Tarehe ya FGD** | |
| **Eneo shule ilipo** | |
| **Jina la Shule** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 1** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 2** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 3** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |

| Taarifa za mshiriki wa 4 | |
|---|---|
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |
| **Taarifa za mshiriki wa 5** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Uzoefu kazini** | |

## Maswali ya mahojiano

1. Una aina gani ya ulemavu au ugonjwa sugu? Je, ni hali iliyopatikana kwa muda au hali ambayo umezaliwa nayo?

   *[Angalizo kwa mtafiti: hakikisha unauliza KILA mshiriki katika kikundi swali hili. Ikiwa mshiriki yeyote hapendi kutaja ugonjwa au ulemavu wake mbele ya wenzake, usimlazimishe. Ikiwezekana, muulize kwa faragha baadaye.]*

2. Ulemavu huu/ugonjwa huu unaathiri vipi utendaji kazi wako wa kila siku shuleni?

   *(Ikiwa hawakutaja JzK, dodosa):* Na unaathiri vipi JzK au MEWAKA?

3. Je, una mahitaji maalum ya ufundishaji au mahitaji mengine yanayohusiana na ulemavu/ugonjwa wako ambayo MEWAKA inaweza kuwa msaada? ?

4. Je, unahisi kuwa unaweza kufika na kushiriki kwenye vikao vya JzK sawa na walimu wengine?

   a. Ikiwa sivyo, ni changamoto gani unakutana nazo?

5. Ni mambo gani yanayokusaidia kushiriki kwenye vikao vya JzK?

a. Nini kinaweza kufanywa ili kuongeza ushiriki wako?

6. Walimu wenye ulemavu wameripoti kwamba vishikwambi, moduli katika LMS, na programu hazitoi msaada wa kutosha kwao.

   a. Je, hili ni tatizo kwako?

   Kama ndiyo:

   b. Ni aina gani maalum za teknolojia saidizi zinaweza kukusaidia kushiriki kikamilifu katika shughuli za MEWAKA?

   c. [Ikiwa haijaelezwa bado] Unafahamu kiasi gani kuhusu aina za vifaa hivyo?

      i. Je, umewahi kuona aina yoyote ya teknolojia saidizi ikitumika?

   d. Unahitaji aina gani ya mafunzo ili kutumia teknolojia hiyo kwa ufanisi?

   e. Una mawazo gani kuhusu nani anaweza kutunza teknolojia hiyo ili iweze kufanya kazi kwa muda mrefu?

7. Je, kuna aina nyingine za msaada katika ngazi ya shule ambazo zinaweza kukusaidia kushiriki katika MEWAKA?

8. [*Eleza*:]Moja ya mapendekezo kutoka katika raundi ya kwanza ya utafiti huu ilikuwa kuimarisha usaidizi kwa walimu wenye ulemavu ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za MEWAKA. Mapendekezo hayo ni pamoja na kuandaa mwongozo toshelevu na jumuishi unaoshughulikia mahitaji na changamoto zako maalum.

   (a) Je, kuna hatua maalumu, miongozo au sera ambazo zitakusaidia zikitekelezwa kwa ngazi ya wilaya, mikoa au serikali kuu?

   (b) [ikiwa hatua hizi mbili hazijatajwa, uliza kuhusu:]

   i) posho za ulemavu kusaidia usafiri,
   ii) kuanzisha mitandao ya walimu wenye ulemavu kati ya shule na shule

   (c) Je, hizi zitakuwa za manufaa?

   (d) Ni changamoto zipi zinaweza kutokea katika utekelezaji wake?

9. Je, kuna mabadiliko yoyote kwenye programu ya MEWAKA yenyewe ambayo yanaweza kukusaidia kushiriki kwa usawa na walimu wengine?

Kama ndiyo, tafadhali eleza.

10. Matokeo ya utafiti wetu katika raundi ya kwanza yalionesha kwamba walimu wengi waliripoti wenyewe kuwa na ulemavu tofauti na takwimu zilizotolewa na wakuu wa shule. Ni sababu zipi unadhani zilisababisha tofauti hii?

11. Inaaminika kwamba walimu wa kike wenye ulemavu wanakumbana na changamoto zaidi kuliko walimu wa kiume wenye ulemavu, kwa sababu walimu wengine wanatoa ushirikiano mdogo kwa walimu wa kike wenye ulemavu. Hali hii ikoje kwa uzoefu wako?

    *(Angalizo kwa Mtafiti: baadhi yao wataeleza uzoefu wa kibinafsi, ikiwa, lakini wengine wataeleza kile walichokiona)*

## Mwisho wa mahojiano

Asanteni nyote kwa muda wenu na kwa kujibu maswali yangu yote - hilo lilikuwa swali langu la mwisho kwenu.

1. Je, kuna kitu kingine chochote ambacho ungependa kuniambia kuhusu MEWAKA/JzK ambacho hatujakijadili?
2. Je, kuna yeyote kati yenu ana swali lolote kwangu kabla hatujamaliza?

***Mwishoni, mpatie Mwalimu Mkuu nakala (A3) ya Matokeo na Mapendekezo.***

**Maoni** - kisanduku hapa chini kitajazwa na watafiti baada ya mahojiano ya kikundi lengwa: Tafadhali andika mawazo yoyote au vidokezo unavyoona ni muhimu kushiriki na timu ya utafiti

| **Maoni ya mtafiti** *(pamoja na mabadiliko)* |
| --- |
| |

# Mwongozo wa majadiliano ya kikundi lengwa cha Mwezeshaji Rika, Mwalimu wa Taaluma na Mwalimu Mkuu

**Lengo**: Kushirikisha matokeo na mapendekezo wa utafiti ya raundi ya kwanza wa ukusanyaji wa data na kukusanya maoni na mrejesho kutoka kwa timu ya MEWAKA.

**Washiriki Walengwa:** Mkuu wa shule, mwezeshaji rika aliyetekeleza JzK iliyotazamwa, mwalimu wa taaluma, na ikiwa shule ina wawezeshaji rika, mmoja au wawili wao wanaweza kujiunga katika mahojiano, ikiwa wanaweza kupatikana.

## Utangulizi na Idhini

**Maelekezo**: Tumia "Hati ya ridhaa ya mdomo ya mshiriki wa utafiti" kutoa utangulizi na kupata idhini kabla ya kuanza mahojiano.

### Taarifa za kurekodi

*Ijazwe na mtafiti kabla ya kuanza FGD*

| | |
|---|---|
| **Mkoa** | |
| **Wilaya** | |
| **Kata** | |
| **Shule** | |
| **Jina la mtafiti** | |
| **Tarehe ya Kikundi Lengwa** | |
| **Participant Details** | |
| **Mshiriki wa 1:**<br>**a. Jina** | |
| **b. JInsi** | |
| **c. Ulemavu unaotambuka** | Ikiwa ndiyo, tafadhali taja |
| **d. Cheo** | Mwezeshaji rika    Mwalimu wa taaluma<br>Mwalimu mkuu |
| **e. Uzoefu kazini** | |

| | |
|---|---|
| **Mshiriki wa 1:**<br>**a. Jina** | |
| **b. JInsi** | |
| **c. Ulemavu unaotambuka** | Ikiwa ndiyo, tafadhali taja |
| **d. Cheo** | Mwezeshaji rika Mwalimu wa taaluma<br>Mwalimu mkuu |
| **e. Uzoefu kazini** | |
| **Mshiriki wa 1:**<br>**a. Jina** | |
| **b. JInsi** | |
| **c. Ulemavu unaotambuka** | Ikiwa ndiyo, tafadhali taja |
| **d. Cheo** | Mwezeshaji rika Mwalimu wa taaluma<br>Mwalimu mkuu |
| **e. Uzoefu kazini** | |

## Muundo wa Kikundi Lengwa cha Mwezeshaji wa Rika, Mwalimu wa Taaluma na Mkuu wa Shule

Kikundi lengwa kina sehemu 2:

1. Matokeo ya raundi ya 1
2. Kuweka kipaumbele mapendekezo ya raundi ya kwanza ya utafiti

Mahojiano yatafanyika kwa takriban dakika 45 hadi 1 saa.

### Maswali ya Majadiliano - PF, AT, HT

## Sehemu ya 1: Matokeo ya Utafiti Raundi ya Kwanza

**Hatua ya 1a: Eleza: K**wanza, tungependa kuwasilisha matokeo muhimu kutoka kwenye raundi ya kwanza ya ukusanyaji wa data na kuyajadili nawe. [*Bandika* karatasi ya matokeo kutoka *raund*i *ya* kwanza *ya* ukusanyaji wa data mahali ambapo washiriki wote wa kikundi lengwa wanaweza kuyaona kwa wazi**.**

***Hatua ya 1b: Eleza*** *kwamba matokeo na mapendekezo yamewasilishwa ngazi ya kitaifa (WIZARA), na tunawasilisha kwa ngazi za kata, wilaya na mkoa pamoja na shuleni.*

**Hatua ya 2: Soma kwa sauti** matokeo makuu huku washiriki wakiangalia toleo lililochapishwa na kubandikwa**:**

Matokeo:

*[Angalizo: Matokeo ya utafiti wetu yamejumuishwa hapa kama mfano - yanapaswa kubadilishwa yawe matokeo ya utafiti wako]*

1. ***Walimu wenye ulemavu:*** *Kati ya walimu 125 (MKOA), walimu 14 waliripoti kuwa na ulemavu uliochunguzwa kitalaamu, na 12 walikuwa na magonjwa sugu kama vile kisukari au pumu. Ni muhimu kutambua kwamba idadi ya walimu wenye ulemavu waliobainisha wenyewe ilikuwa kubwa zaidi kuliko ile iliyotolewa na walimu wakuu. Walimu wenye ulemavu waliripoti kwamba vishikwambi, moduli kutoka katika mfumo wa ujifunzaji (LMS), na programu hazina msaada wa kutosha kwa wenzao wenye uoni hafifu.*

2. ***Mabadiliko****: Shule zilizo na walimu wenye ulemavu zilitumia mikakati mbalimbali ili kuongeza usawa katika ushiriki katika jumuiya za ujifunzaji, ikiwa ni pamoja na kutumia mbinu za ushirikiano na uchangamani (kama vile mijadala), kusaidia walimu wenye ulemavu kushiriki, na kuhakikisha mawasiliano yanakuwa wazi. Hakuna marekebisho ya matini za ujifunzaji zilizobainishwa. Pia wadau walibaini kutokuwepo kwa mwongozo wa namna ya kutoa msaada kwa walimu wenye ulemavu.*

3. ***Ushiriki wenye usawa wa kijinsia katika JzK:*** *Ni asilimia 38 tu ya wawezeshaji rika walikuwa wanawake. Walimu wa kiume na wa kike hushiriki kwa usawa katika vikao vingi (8 kati ya 12) vya JzK. Aidha, katika shule 4 kati ya 12, kulikuwa na ukosefu wa ushiriki sawa. Vizuizi vinavyohusiana na jinsia vilivyobainishwa ni pamoja na umakini mdogo wa wawezeshaji rika katika kuhakikisha walimu wote wanashiriki kwa usawa. Katika JzK zilizokosa ushiriki kwa usawa, mara nyingi ushiriki wa walimu wa kike ulikuwa mdogo hasa katika vipindi vinavyohusiana na teknolojia.*

4. ***Uwezo wa kukidhi mahitaji ya walimu:*** *Walimu wanakidhi mahitaji yao kupitia njia zifuatazo: i) kuweka vipaumbele vya JzK, ii) kutumia data za simu za mkononi katika MEWAKA, na iii) kutoa msaada wa kiteknolojia kwa wenzao. Baadhi ya shule zilitoa vifurushi vya intaneti au chakula kwa walimu. Pia Mthibiti Ubora wa Wilaya moja alianzisha kundi la WhatsApp la walimu. Hata hivyo, karibu washiriki wote waliona kuwa walimu wana nafasi ndogo ya kufanya maamuzi, na shule kadhaa zilihisi kuwa hazikuwa na msaada ikiwa mahitaji ya kiufundishaji ya walimu yasingeweza kutatuliwa ndani ya shule.*

5. ***Taratibu zinazoruhusu mrejesho ili kukidhi mahitaji ya walimu:*** *Taratibu zimewekwa ili kubadilisha shughuli za JzK ili kukidhi mahitaji ya walimu ndani ya shule na kata, ikiwa ni pamoja na kushughulikia*

*changamoto na kueneza ubunifu. Hata hivyo, mkoa wa (MKOA) pekee ndiyo uliokuwa na utaratibu wa kutoa mrejesho na kuufanyia kazi kikamilifu kuanzia ngazi ya shule, kata, Kituo cha Walimu (TRC) na wilaya.*

6. ***Mahitaji ya walimu ambayo hayawezi kutatuliwa katika ngazi ya shule kwa kiasi kikubwa yanabaki bila msaada.*** *Kwa mfano, mahitaji ya miundombinu ya mawasiliano, pamoja na ukosefu wa vifaa, ujuzi mdogo wa kidijitali wa walimu, upatikanaji wa vifaa vya teknolojia saidizi kwa walimu wenye ulemavu, gharama za data, kukosekana kwa mtandao, na matatizo ya upatikanaji na matumizi ya LMS.*

**Hatua ya 3: *uliza kundi:***

- **Swali 1:** Je, mna swali lolote la ufafanuzi kabla hatujaanza shughuli? *[Subiri ili kujibu maswali yoyote] Sasa tutafanya shughuli ili kupata maoni yenu kuhusu matokeo tuliyowashirikisha.*

  *[ANGALIZO: hakikisha maswali ni yale **yanayofafanua** maudhui yaliyowasilishwa. Ikiwa washiriki wanataka kutoa mawazo/maoni yao, eleza kuwa watapata nafasi ya kufanya hivyo katika shughuli inayofuata.]*

**Hatua ya 4: *Sitisha kurekodi na mpe kila mshiriki vidakuzi na kalamu***(*kalamu za rangi nyeusi kwa wanawake, kalamu za bluu/nyekundu kwa wanaume). Gawa **bango kitita moja** (kwa ajili ya kundi).*

**Hatua ya 5: Eleza:** "Nitawauliza maswali kadhaa. Kwa kila swali, ningependa kila mmoja wenu aandike jibu lake mwenyewe kwenye kidakuzi. Tafadhali andika jibu lako mwenyewe kwenye kidakuzi tofauti kwa kila swali. (yaani kwenye kila kidakuzi kuna jibu moja tu)."

- **Swali 2:** Ni mawazo gani ya kwanza yalikujia baada ya kusikia matokeo haya? *[Subiri li kuwapa washiriki muda wa kuandika jibu lao kwenye kidakuzi]*
- **Swali 3:** Ni matokeo gani yalikugusa zaidi? Kwa nini? *Subiri ili kuwapa washiriki muda wa kuandika jibu lao kwenye kidakuzi]*

**Hatua ya 6: Anza tena kurekodi na Eleza:** "Sasa wekeni vidakuzi vyenu kwenye bango kitita, angalia majibu ya wengine na jadiliana mawazo yenu. Mmoja atusomee kwa sauti" ***<u>Hakikisha unaanza kurekodi tena.</u>***

**Hatua ya 7: Maswali ya ufuatiliaji**

- **Swali 4:** *[Uliza kama hayakujadiliwa wakati wa Swali la 3*] Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, kulikuwa na tofauti kati ya idadi ya walimu wenye ulemavu iliyowasilishwa na walimu wakuu na iliyotolewa na walimu wenyewe. Je, una maoni gani kuhusu hali hii?
  - a. *Dodoso ikiwa haijajibiwa:*
    - i. Je, ulishtuka kusikia kuwa walimu zaidi waliripoti kuwa na ulemavu kuliko ile idadi iliyotolewa na wakuu wa shule?

ii. Unafikiri ni nini inasababisha tofauti hizi (za takwimu/idadi)?

- **Swali 5:** *[ikiwa matokeo kuhusu jinsia hayajadiliwa anza na swali hili]:* Je, una maoni yoyote kuhusu matokeo yanayohusiana na jinsia ambayo umeyasikia hivi punde?

  a. Dodosa:

  i. Je, mlishangaa kusikia kuwa wanawake wanashiriki kidogo zaidi katika mikutano ya JzK inayohusiana na teknolojia?

  ii. Kwa nini unafikiria hali iko hivyo?

  1. [Ikiwa hawakugusia haya, uliza:] Utafiti umeonyesha kuwa wanawake na wasichana wana uwezekano mdogo wa kumiliki na kutumia vifaa vya teknolojia kuliko wanaume na wavulana. Je, unafikiria hili linaathiri walimu wa kike?

  iii. Unafikiria nini kinaweza kufanywa ili kushughulikia hili?

**Hatua 8: Uliza Swali la sita, na ikiwa wanataja mambo mengine, waambie waandike kwenye vidakuzi na wabandike vidakuzi hivo kwenye bango kitita mpya.** Idadi isizidi vidakuzi 3 kwa mtu mmoja.

- Swali 6: Je, kuna mambo mengine ambayo unafikiri hayakutajwa kwenye matokeo wasilisho hili

***NB: Washukuru kwa kuibua masuala zaidi ambayo hayajagusiwa vya kutosha kwenye matokeo*** *Weka lebo kwenye bango kitita yenye tarehe, , na namba ya shule (ID) kisha chukua picha ya kila bango kitita. Hifadhi picha na ziweke kwenye nakala ya majadiliano.*

## Sehemu ya II. Kuweka Kipaumbele Mapendekezo ya Raundi ya Kwanza ya Utafiti [dakika 20]

**[Sitisha kurekodi mpaka hatua ya 4]**

**Hatua ya 1:** ***Bandika mapendekezo*** *[large print] mahali ambapo washiriki wanaweza kuyaona.*

**Hatua ya 2:** ***Eleza*** *kwamba kulikuwa na mapendekezo kadhaa kulingana na matokeo ya raundi ya kwanza* ***na zungumzia*** *kwa kifupi (wasilisha) mapendekezo haya.*

***Baada ya kuwasilishwa , uliza:*** Soma tu vipengele vya msingi kisha uliza kama kuna maswali yoyote ya ufafanuzi wa mapendekezo hayo.

Mapendekezo:

*[Angalizo: Mapendekezo ya utafiti wetu yamejumuishwa hapa kama mfano - yanapaswa kubadilishwa na mapendekezo ya utafiti wako]*

**Taratibu Saidizi:**

1. Kuongeza ufahamu wa moduli za JzK: Hakikisha kwamba wadau wote (wakuu wa shule, wawezeshaji rika, WEOs, na DSQAOs, n.k.) wanaelewa asili ya muktadha wa MEWAKA na wana vifaa vya kutosha kusaidia na kutekeleza MEWAKA katika ngazi ya shule.

2. Kukuza na kutekeleza taratibu za kutoa mrejesho wa mahitaji ya walimu: Kushughulikia mahitaji ya walimu ambayo hayajatatuliwa katika ngazi ya shule na kuwawezesha kusambaza maarifa na kuiga ubunifu katika MEWAKA kati ya shule moja na nyingine. Hii inaweza kujumuisha:
    a. Kuwa na mifumo bora ya kusaidia shule/walimu wanapokutana na changamoto katika utekelezaji wa JzK/MEWAKA.
    b. Kuhakikisha usambazaji endelevu wa bunifu zenye ufanisi katika ya shule zote.

**Miundombinu na Teknolojia:**

3. Kuongeza upatikanaji wa moduli za JZK kwa shule zenye mtandao za intaneti ambazo ni hafifu kwa kutathmini na kujaribisha utekelezaji wa upatikanaji wa moduli bila kutumia mtandao (offline) na/au kutafuta upatikanaji wa bure wa LMS kwa walimu kupitia watoa huduma wa mitandao ya simu.

4. Kutekeleza upatikanaji wa umeme wa jua kwa shule zisizo na umeme ili kuwawezesha walimu kuzifikia LMS na moduli za JzK.

5. Kukuza tabia za kuazimana vifaa vya teknolojia baina ya walimu katika ngazi ya shule.

6. Kuchambua changamoto zinazojitokeza katika matumizi ya vishikwambi vilivyotolewa hivi karibuni kwa walimu katika muktadha mbalimbali wa shule.

**Usawa: Walimu wenye Ulemavu**

7. Kupanua dhana na ubainishaji wa ulemavu ili kuhakikisha kwamba takwimu za elimu zinakusanywa kwa usahihi. Hii ikijumuisha taarifa za walimu wenye ulemavu wa kuona, kusikia, na kutembea, na pia kuhusisha ulemavu wa aina nyingine, kwa mfano ulemavu wa akili.

8. Kurasimisha utoaji wa msaada kwa walimu wenye ulemavu ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za MEWAKA kwa kuandaa mwongozo toshelevu na jumuishi utakaoshughulikia mahitaji yao na changamoto zao maalumu. Pia kutoa teknolojia saidizi kama za usomaji wa skrini, kuandaa ruzuku za walemavu ili kusaidia usafiri, na kuanzisha mitandao ya walimu wenye ulemavu kati ya shule na shule.

**Usawa: Jinsia**

9. Kuweka mikakati ya kuongeza ushiriki wa walimu wa kike katika vikao na shughuli za JzK. Hii inaweza kujumuisha:
    a. Kuteua Maafisa wa TEHAMA wa Wilaya na mabingwa wa TEHAMA wa shule kuwa na jukumu la kusaidia walimu wenye ujuzi mdogo wa kidijitali kutumia LMS na vishikwambi vilivyotolewa na serikali.
    b. Kuwepo mwongozo na ufuatiliaji ili kuhakikisha idadi ya wawezeshaji rika wa kike na wa kiume inalingana.
    c. Kuandaa warsha na mafunzo maalum ili kuwasilisha na kushughulikia matokeo kuhusu ushiriki wa jinsia na utofauti uliopo.

**Hatua ya 3: *Gawa kadi*** *za mapendekezo* ***na waelekeze washiriki kupanga mapendekezo*** *kutokana na umuhimu au kipaumbele yake - yapi ni muhimu zaidi na yanapaswa kushughulikiwa kwanza, ili kuendelea kuboresha MEWAKA.*

- **Wafanye kwa pamoja kama kundi,** yaani wajadiliane ili kufikia makubaliano kuhusu mpangilio.
- Waambie kuweka kadi katika mpangilio, kuanzia **1 ikiwa kipaumbele cha muhimu zaidi hadi 9 kama kipaumbele cha chini zaidi.**

**Hatua ya 4: Anza tena kurekodi** baada ya kuwa wamepanga kadi kwa mpangilio wa kipaumbele.

**Hatua ya 5: Maswali ya majadiliano**

a. Kwa nini X [soma kadi yao ya kipaumbele cha #1] ni pendekezo muhimu zaidi?

b. Je, Kuna mahali mlitofautiana (kuhusu mpangilio)? Kama ndiyo, eleza kwa kifupi.

c. Je, kuna mapendekezo mengine yoyote ungependa kuongeza?

***NB:*** *Weka kidakuzi chenye tarehe na namba ya shule na jina la kundi (PF/AT/HT au "TCPD team") karibu na mpangilio wa kadi za kundi, kisha piga picha za kadi za mapendekezo zilizopangwa. Hifadhi picha hiyo na hakikisha inaingizwa katika maandiko ya kikundi lengwa.*

## Mwisho wa mahojiano

Asanteni nyote kwa muda wenu na kwa kujibu maswali yangu yote - hilo lilikuwa swali langu la mwisho kwenu.

1. Je, kuna kitu kingine chochote chochote ambacho ungependa kuniambia kuhusu MEWAKA/JzK ambacho hatujakijadili?
2. Je, kuna yeyote kati yenu ana swali lolote kwangu kabla hatujamaliza?

*Mwishoni, mpatie Mwalimu Mkuu nakala (A3) ya Matokeo na Mapendekezo.

**Maoni** - Sanduku hapa chini litajazwa na watafiti baada ya mahojiano na mwezeshaji rika na mwalimu wa taaluma; tafadhali andika maoni au vidokezo vyovyote muhimu ambavyo unadhani vinapaswa kushirikiwa na timu ya utafiti.

| **Maoni ya mtafiti** *(pamoja na mabadiliko)* |
|---|
| |

# Usaili wa Wahabarishaji Muhimu Raundi ya pili

**Lengo:** Kuelewa viwezeshi, vikwazo na mabadilko ya MEWAKA katika ngazi mbalimbali za utawala.

## Mwongozo wa mahojiano na mwakilishi wa serikali kuu

### Utangulizi na Idhini

Maelekezo: Tumia "Hati ya ridhaa ya mdomo ya mshiriki wa utafiti" ili kutoa utangulizi na kupata idhini kabla ya kuanza mahojiano.

### Taarifa za kurekodi

*Ijazwe na mtafiti kabla ya kuanza mahojiano*

| | |
|---|---|
| **Jina la mtafiti** | |
| **Tarehe ya Mahojiano** | |
| **Mahali pa mahojiano [ana kwa ana/ki umbali]**<br>*(ikiwa ana kwa ana, kumbuka mahali)* | |
| **Taarifa za Mshiriki** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Taasisi** | MoEST PO-RALG Other (specify): |
| **Jukumu** | |
| **Idadi ya miaka katika jukumu hili** | |

## Muundo wa Mahojiano

Majadiliano katika mahojiano haya yatachunguza: Jinsi maudhui ya MEWAKA, muundo na utaratibu unavyorekebishwa katika miktadha tofauti (RQ1), Jinsi mahitaji mbalimbali na ushiriki sawa wa vikundi mbalimbali vya walimu unavyosaidiwa katika MEWAKA (RQ2), na mafanikio na changamoto za utekelezaji wa MEWAKA katika kiwango cha kitaifa(RQ3).

Majadiliano haya yatachukua takribani dakika 45.

### Mahojiano na mwakilishi wa serikali kuu

1. Kuanzia Machi mwaka huu, je, una ufahamu wa mikakati mipya ya motisha iliyotumiwa na wewe mwenyewe au maafisa elimu wa mkoa kuwahimiza walimu kushiriki katika Jumuiya za Kujifunza (JzK)?

   Ikiwa ndiyo,

   a. Tafadhali eleza mikakati iliyotumika.

   b. Je, mikakati hii imekuwa na mafanikio kwa kiwango gani?

2. Je, umewahi kuona au kusikia kuhusu uvumbuzi au mazoea mazuri katika mkoa mmoja ambayo ulifikiri wengine wanapaswa kufuata?

   Ikiwa ndiyo,

   a. Ulisikiaje kuhusu hilo? *(Angalizo kwa mtafiti: fahamu njia za maoni/mrejesho zilizotumiwa na uone kama zilikuwa za kimfumo au kwa bahati tu.)*

   b. Na ulichukua hatua gani kuhusu hilo? (Au kama hujafanya chochote bado): Kama ungependa kueneza uvumbuzi huo kwa mikoa mingine, ungefuata mchakato gani?

3. Kuanzia Machi mwaka huu, je, kumekuwa na mabadiliko yoyote yaliyoonekana au marekebisho ya namna shule zinavyoipokea au kutekeleza MEWAKA ambayo umeyabaini?

   Ikiwa ndiyo, tafadhali fafanua.

   a. Umejua kwa njia gani kuhusu tofauti au marekebisho haya? (Chunguza – je, yameripotiwa rasmi kwenye mikutano au ripoti za maandishi)? Je, ni kutokana na uchunguzi wao wenyewe kwa kutembelea/kuzungumza na shule tofauti? N.k.)

   b. Kwa maoni yako, ni mambo gani yanaweza kutofautiana kati ya shule moja na nyingine katika utekelezaji wake? [mfano: unyumbufu (flexibility) katika ratiba [scheduling] za JzK]?

4. Katika raundi ya kwanza ya utafiti, ilionekana kuwa baadhi ya shule zina walimu wenye ujuzi mdogo wa kidijitali na walimu wengine wenye ulemavu au magonjwa sugu. Je, kuna taratibu zozote katika ngazi ya taifa kusaidia walimu hawa kushiriki kwa usawa katika shughuli za JzK/MEWAKA?
    a. Ikiwa ndio, tafadhali eleza taratibu za usaidizi zilizopo.
    b. Je, zimekuwa na mafanikio kiasi gani?
    c. (Kama haijatajwa hapo awali:) Inaonekana kuwa walimu wengi hawatumii moduli za JzK kutokana na ukosefu wa uzoefu au ujuzi wa kutumia teknolojia, hata pale wanapokuwa na mtandao; wanapata ugumu kufikia LMS au kutumia vishkwambi vilivyokishwatumika katika sensa. Je, kuna hatua zozote za kuwafunza au kuwasaidia walimu katika eneo hili? (Kama haijajadiliwa tayari: Je, pendekezo kuhusu kuteua "ICT champions" lingeendana na hili, ili kusaidia kupunguza gharama kwa kutoa msaada wa ndani kwa kutumia wafanyakazi waliopo?) Ikiwa ndiyo, ni hatua gani zinazofuata na ratiba ya kutoa mafunzo au msaada?
5. Walimu katika utafiti wetu waliripoti changamoto za kutumia teknolojia kutokana na ukosefu wa mtandao wa intaneti na vifaa vya kiteknolojia visivyotosha, hasa teknolojia saidizi kwa walimu wenye ulemavu kama vile vipofu. Je, kuna mifumo yoyote ya kitaifa iliyopo kusaidia walimu wanaokumbana na changamoto hizi katika kutumia teknolojia kwa ufanisi kwa ajili ya MEWAKA?
    a. Ikiwa kuna, tafadhali eleza mifumo hii iliyopo.
    b. Je, mifumo hii imekuwa na mafanikio kwa kiwango gani?
    c. Moja ya uchunguzi maalum ilikuwa kwamba walimu wenye ulemavu waliripoti kutokuwa na programu za kusoma skrini (screen readers), hali ya kuwa programu za bure za aina hii zinaonekana kupatikana. Je, kuongeza ufahamu na kusaidia matumizi ya teknolojia hii kunaweza kufanywa, ili kuboresha ufikiaji wa matini za moduli za JzK?
    d. Pia tunaelewa kuwa moduli mpya za CoL zitatengenezwa kwa Braille, lakini seti ya awali ya moduli 12 haikutengenezwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Je, kuna jitihada zaidi ambazo zinaweza kufanyika ili kutengeneza nyenzo maalumu kwa walimu wenye ulemavu?
    e. Je, kuna maendeleo gani ya sasa kuhusu utekelezaji wa intaneti bila malipo kwa walimu?

## Mwisho wa mahojiano

Asante kwa muda wako na kwa kujibu maswali yangu yote - hilo lilikuwa swali langu la mwisho kwenu.

1. Je, kuna kitu kingine chochote ambacho ungependa kunishirikisha kuhusu uzoefu wako ambacho hatujajadili?

2. Je, una swali lolote kwangu kabla hatujamaliza?

Maoni — kisanduku kilicho hapa chini kitajazwa na wadadisi kufuatia uchunguzi uliofanywa, tafadhali andika tafakuri au madokezo yoyote ambayo unafikiri ni muhimu kushirikishwa kwa[TAASISI HUSIKA], au washirika wengine.

**Maoni ya mtafiti** *(jumuisha mabadiliko yoyote yaliyofanyika)*

# Mwongozo wa usaili kwa Afisa Elimu Taaluma wa Mkoa (RAO)

## Utangulizi na Idhini

Maelekezo: Tumia "Hati ya ridhaa ya mdomo ya mshiriki wa utafitii" ili kutoa utangulizi na kupata idhini kabla ya kuanza mahojiano. **HALI KADHALIKA, KAMA AFISA HUYU HAJAWAHI KUHOJIWA KATIKA UTAFITI WETU FUATILIA WRITTEN CONSENT.**

## Taarifa za Kurekodi

*Ijazwe na mtafiti kabla ya kuanza mahojiano*

| | |
|---|---|
| **Jina la mtafiti** | |
| **Tarehe ya Mahojiano** | |
| **Mkoa** | |
| **Maelezo ya Mshiriki** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Jukumu** | |
| **Muda ambao amefanya kazi hii [this role]** | Miaka _____ |
| **Ana ulemavu wowote unaojulikana?** | Kama ndiyo, tafadhali onesha: ____________________ |

## Muundo wa Mahojiano

Mahojiano haya yana sehemu tatu ambazo tutazipitia pamoja:

- Sehemu ya 1: Matokeo ya Utafiti ya Raundi ya Kwanza
- Sehemu ya 2: Kuweka kipaumbele Mapendekezo ya Raundi ya Kwanza

- Sehemu ya 3: Mabadiliko katika MEWAKA (adaptations)

Majadiliano yatachunguza: Jinsi maudhui ya MEWAKA, muundo na njia za programu ya MEWAKA yanavyorekebishwa kulingana katika muktadha tofauti (RQ1), Jinsi mahitaji mbalimbali na ushiriki sawa wa vikundi tofauti vya walimu vinavyosaidiwa katika MEWAKA (RQ2), na mafanikio na changamoto za utekelezaji wa MEWAKA kwa kiwango cha kitaifa (RQ3.)

Mjadala huu utachukua takriban dakika 45 hadi saa 1.

---

## Mahojiano ya Afisa Elimu wa Mkoa

### Sehemu ya 1: Matokeo ya Utafiti ya Raundi ya Kwanza

**Hatua ya 1: Eleza:** Kwanza, tungependa kuwasilisha matokeo muhimu ya raundi ya kwanza ya ukusanyaji wa data na kuyajadili pamoja nanyi**. *[Onesha karatasi ya A3 yenye matokeo]***

**1b: Eleza** kwamba matokeo na mapendekezo yamewasilishwa ngazi ya kitaifa (*WIZARA*), na tunawasilisha kwa ngazi za kata, wilaya na mkoa pamoja na shuleni.

**Hatua ya 2: Wasilisha (kwa kifupi) matokeo makuu** huku mshiriki akitazama matokeo yaliyochapishwa**.**

<u>Matokeo:</u>

*[Angalizo: Matokeo ya utafiti wetu yamejumuishwa hapa kama mfano - yanapaswa kubadilishwa yawe matokeo ya utafiti wako]*

1. ***Walimu wenye ulemavu:*** Kati ya walimu 125 kutoka (MKOA), walimu 14 waliripoti kuwa na ulemavu uliochunguzwa kitalaamu, na 12 walikuwa na magonjwa sugu kama vile kisukari au pumu. Ni muhimu kutambua kwamba idadi ya walimu wenye ulemavu waliobainisha wenyewe ilikuwa kubwa zaidi kuliko ile iliyotolewa na walimu wakuu. Walimu wenye ulemavu waliripoti kwamba vishikwambi, moduli kutoka katika mfumo wa ujifunzaji (LMS), na programu hazina msaada wa kutosha kwa wenzao wenye uoni hafifu.
2. ***Mabadiliko:*** Shule zilizo na walimu wenye ulemavu zilitumia mikakati mbalimbali ili kuongeza usawa katika ushiriki katika jumuiya za ujifunzaji, ikiwa ni pamoja na kutumia mbinu za ushirikiano na uchangamani (kama vile mijadala), kusaidia walimu wenye ulemavu kushiriki, na kuhakikisha mawasiliano yanakuwa wazi. Hakuna marekebisho ya matini za ujifunzaji zilizobainishwa. Pia wadau walibaini kutokuwepo kwa mwongozo wa namna ya kutoa msaada kwa walimu wenye ulemavu.

3. ***Ushiriki wenye usawa wa kijinsia katika JzK:*** Ni asilimia 38 tu ya wawezeshaji rika walikuwa wanawake. Walimu wa kiume na wa kike hushiriki kwa usawa katika vikao vingi (8 kati ya 12) vya JzK. Aidha, katika shule 4 kati ya 12, kulikuwa na ukosefu wa ushiriki sawa. Vizuizi vinavyohusiana na jinsia vilivyobainishwa ni pamoja na umakini mdogo wa wawezeshaji rika katika kuhakikisha walimu wote wanashiriki kwa usawa. Katika JzK zilizokosa ushiriki kwa usawa, mara nyingi ushiriki wa walimu wa kike ulikuwa mdogo hasa katika vipindi vinavyohusiana na teknolojia.

4. ***Uwezo wa kukidhi mahitaji ya walimu:*** Walimu wanakidhi mahitaji yao kupitia njia zifuatazo: i) kuweka vipaumbele vya JzK, ii) kutumia data za simu za mkononi katika MEWAKA, na iii) kutoa msaada wa kiteknolojia kwa wenzao. Baadhi ya shule zilitoa vifurushi vya intaneti au chakula kwa walimu. Pia Mthibiti Ubora wa Wilaya moja alianzisha kundi la WhatsApp la walimu. Hata hivyo, karibu washiriki wote waliona kuwa walimu wana nafasi ndogo ya kufanya maamuzi, na shule kadhaa zilihisi kuwa hazikuwa na msaada ikiwa mahitaji ya kiufundishaji ya walimu yasingeweza kutatuliwa ndani ya shule.

5. ***Taratibu zinazoruhusu mrejesho ili kukidhi mahitaji ya walimu:*** Taratibu zimewekwa ili kubadilisha shughuli za JzK ili kukidhi mahitaji ya walimu ndani ya shule na kata, ikiwa ni pamoja na kushughulikia changamoto na kueneza ubunifu. Hata hivyo, mkoa wa (MKOA) pekee ndiyo uliokuwa na utaratibu wa kutoa mrejesho na kuufanyia kazi kikamilifu kuanzia ngazi ya shule, kata, Kituo cha Walimu (TRC) na wilaya.

6. ***Mahitaji ya walimu ambayo hayawezi kutatuliwa katika ngazi ya shule kwa kiasi kikubwa yanabaki bila msaada.*** Kwa mfano, mahitaji ya miundombinu ya mawasiliano, pamoja na ukosefu wa vifaa, ujuzi mdogo wa kidijitali wa walimu, upatikanaji wa vifaa vya teknolojia saidizi kwa walimu wenye ulemavu, gharama za data, kukosekana kwa mtandao, na matatizo ya upatikanaji na matumizi ya LMS.

**Uliza**: Je, kuna maswali yoyote ya ufafanuzi wa mapendekezo haya?

### Hatua ya 3: Uliza maswali

1. Ni mawazo gani ya kwanza yalikujia baada ya kusikia matokeo haya?
2. Nini kimekugusa zaidi kutoka kwenye matokeo haya?

### Hatua ya 4: Maswali ya ufuatiliaji

3. Je, una maoni gani kuhusu matokeo yanayohusiana na jinsia?

Dodosa:

i. Je, ulishangaa kusikia kwamba wanawake wanashiriki kidogo zaidi katika mikutano inayohusiana na teknolojia?

ii. Ni kwanini unadhani ipo hivyo?

   1. *[Ikiwa hawajazungumzia, uliza:*] Utafiti umeonyesha kwamba wanawake na wasichana wana uwezekano mdogo wa kumiliki

na kutumia vifaa vya teknolojia ikilinganishwa na wanaume na wavulana. Je, unaamini kwamba hili linaathiri walimu wa kike?

iii. Ni hatua gani ungependa zichukuliwe ili kushughulikia hali hii?

## Sehemu ya II. Kuweka Kipaumbele Mapendekezo ya Raundi ya Kwanza ya Utafiti

**[dakika 20]**

**Hatua ya 1: Eleza** kwamba kulikuwa na mapendekezo kadhaa kulingana na matokeo ya raundi ya kwanza. Onesha nakala ya mapendekezo mahali ambapo mshiriki atayaona vizuri.

[Unaweza sitisha kurekodi hadi hatua ya 5]

**Hatua ya 2: Soma kwa kifupi** mapendekezo haya.

*[Angalizo: Mapendekezo ya utafiti wetu yamejumuishwa hapa kama mfano - yanapaswa kubadilishwa na mapendekezo ya utafiti wako]*

**Taratibu Saidizi:**

10. Kuongeza ufahamu wa moduli za JzK: Hakikisha kwamba wadau wote (wakuu wa shule, wawezeshaji rika, WEOs, na DSQAOs, n.k.) wanaelewa asili ya muktadha wa MEWAKA na wana vifaa vya kutosha kusaidia na kutekeleza MEWAKA katika ngazi ya shule.

11. Kukuza na kutekeleza taratibu za kutoa mrejesho wa mahitaji ya walimu: Kushughulikia mahitaji ya walimu ambayo hayajatatuliwa katika ngazi ya shule na kuwawezesha kusambaza maarifa na kuiga ubunifu katika MEWAKA kati ya shule moja na nyingine. Hii inaweza kujumuisha:
    a. Kuwa na mifumo bora ya kusaidia shule/walimu wanapokutana na changamoto katika utekelezaji wa JzK/MEWAKA.
    b. Kuhakikisha usambazaji endelevu wa bunifu zenye ufanisi katika ya shule zote.

**Miundombinu na Teknolojia:**

12. Kuongeza upatikanaji wa moduli za JZK kwa shule zenye mtandao za intaneti ambazo ni hafifu kwa kutathmini na kujaribisha utekelezaji wa upatikanaji wa moduli bila kutumia mtandao (offline) na/au kutafuta upatikanaji wa bure wa LMS kwa walimu kupitia watoa huduma wa mitandao ya simu.

13. Kutekeleza upatikanaji wa umeme wa jua kwa shule zisizo na umeme ili kuwawezesha walimu kuzifikia LMS na moduli za JzK.

14. Kukuza tabia za kuazimana vifaa vya teknolojia baina ya walimu katika ngazi ya shule.

15. Kuchambua changamoto zinazojitokeza katika matumizi ya vishikwambi vilivyotolewa hivi karibuni kwa walimu katika muktadha mbalimbali wa shule.

**Usawa: Walimu wenye Ulemavu**

16. Kupanua dhana na ubainishaji wa ulemavu ili kuhakikisha kwamba takwimu za elimu zinakusanywa kwa usahihi. Hii ikijumuisha taarifa za walimu wenye ulemavu wa kuona, kusikia, na kutembea, na pia kuhusisha ulemavu wa aina nyingine, kwa mfano ulemavu wa akili.

17. Kurasimisha utoaji wa msaada kwa walimu wenye ulemavu ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za MEWAKA kwa kuandaa mwongozo toshelevu na jumuishi utakaoshughulikia mahitaji yao na changamoto zao maalumu. Pia kutoa teknolojia saidizi kama za usomaji wa skrini, kuandaa ruzuku za walemavu ili kusaidia usafiri, na kuanzisha mitandao ya walimu wenye ulemavu kati ya shule na shule.

**Usawa: Jinsia**

18. Kuweka mikakati ya kuongeza ushiriki wa walimu wa kike katika vikao na shughuli za JzK. Hii inaweza kujumuisha:
    d. Kuteua Maafisa wa TEHAMA wa Wilaya na mabingwa wa TEHAMA wa shule kuwa na jukumu la kusaidia walimu wenye ujuzi mdogo wa kidijitali kutumia LMS na vishikwambi vilivyotolewa na serikali.
    e. Kuwepo mwongozo na ufuatiliaji ili kuhakikisha idadi ya wawezeshaji rika wa kike na wa kiume inalingana.
    f. Kuandaa warsha na mafunzo maalum ili kuwasilisha na kushughulikia matokeo kuhusu ushiriki wa jinsia na utofauti uliopo.

**Hatua ya 3: Mpe RAO kadi zenye mapendekezo na mwelekeze** kupanga mapendekezo kutokana na umuhimu au kipaumbele yake - yapi ni muhimu zaidi na yanapaswa kushughulikiwa kwanza, ili kuendelea kuboresha MEWAKA.

[1 ikiwa kipaumbele cha juu zaidi au muhimu zaidi hadi 9 ikiwa kipaumbele cha chini zaidi]

**Hatua ya 4: Baada ya RAO kupanga kadi kwa mpangilio wa kipaumbele, ANZA TENA KUREKODI na kuuliza:**

1. Kwa nini X [soma kadi ya kipaumbele cha #1] ni pendekezo muhimu zaidi?

2. Je, kulikuwa na mapendekezo yoyote ambayo yalikupa shida katika kupanga vipaumbele kwa sababu yana umuhimu sawa? Kama ndio, eleza kwa kifupi.

3. Je, kuna mapendekezo ya ziada unayoweza kuyatoa?

*[Dokezo: Kabla ya kupiga picha ya kadi, zipe namba kwa mpangilio wa kipaumbele cha RAO, ukitumia kalamu rashasha inayofutika]*

**NB:** Weka kidakuzi chenye "RAO" tarehe na mkoa karibu na mpangilio wa kadi, kisha piga picha za kadi za mapendekezo zilizopangwa. Hifadhi picha hiyo na hakikisha inaingizwa katika transcript.

---

**Sehemu ya III. Maswali kuhusu ufuatiliaji na mabadiliko**

1. Je, tangu mwezi Machi mwaka huu, ofisi yako, maafisa wa elimu wilaya, au maafisa elimu kata katika mkoa wako mmetumia mikakati yoyote mipya ya kuhamasisha walimu kushiriki katika JzK?

   Ikiwa ndio:

   a. Tafadhali eleza mikakati  hiyo inavyotumika.
   b. Je, mikakati hii imekuwa na mafanikio kiasi gani?

2. Je, umewahi kuona ubunifu au vitendo vizuri vya MEWAKA katika shule moja, kata au TRC ambavyo ulipenda shule nyingine waige? (Kwa mfano, utengenezaji wa vifaa vya kufundishia)

   Ikiwa ndio:

   a. Je, ulifanya nini ili wengine waweze kuiga mfano huu au mifano hiyo?
      i. Ikiwa bado hujalifanyia kazi, ungefuata taratibu zipi  ili wengine waige? Ikiwa bado hujalifanyia kazi, ungefuata taratibu zipi  ili wengine waige?

2. Je, tangu mwezi Machi mwaka huu, kumekuwa na mabadiliko yoyote yanayoonekana katika utekelezaji wa MEWAKA shuleni? (kama vile mabadiliko katika miundo ya vipindi vya JzK au ratiba)

   Ikiwa ndio tafadhali eleza.

   a. Je, unapataje taarifa kuhusu mabadiliko hayo au kuhusu vitendo vizuri katika utekelezaji wa MEWAKA?
      (Dodosa, mf:
      - Je, inaripotiwa rasmi - katika mikutano au ripoti?
      - Je, ni ufauatiliaji wako mwenyewe kwa kutembelea/kuzungumza na shule tofauti? (n.k.)
   b. Kwa maoni yako, ni mambo gani yanaweza kutofautiana kati ya shule moja na nyingine katika utekelezaji wake?   [mfano: unyumbufu (flexibility) katika ratiba [scheduling] za JzK]

3. Katika raundi ya kwanza ya utafiti, ilionekana kuwa baadhi ya shule zina walimu wenye ujuzi mdogo wa kidijitali na walimu wengine wenye

ulemavu au magonjwa sugu. Je, kuna taratibu yoyote katika ngazi ya mkoa kusaidia walimu hawa kushiriki kwa usawa katika shughuli za JzK/MEWAKA?

   a. Ikiwa ndio, tafadhali eleza taratibu za usaidizi uliopo.

   b. Je, umekuwa na mafanikio kiasi gani?

4. Mwezi Machi mwaka huu, walimu waliripoti kuwa wanapata changamoto katika kutumia teknolojia kutokana na ukosefu wa upatikanaji wa intaneti, ujuzi mdogo wa kidijitali, na uhaba vifaa vya teknolojia, hasa kwa wale wenye ulemavu kama vile uoni hafifu. Je, kuna taratibu zozote zimewekwa katika ngazi ya mkoa kusaidia walimu wanaokumbana na changamoto hizi katika kutumia teknolojia kwa ufanisi katika MEWAKA?
   a. Ikiwa ndio, tafadhali eleza taratibu za usaidizi uliopo.
   b. Je, umekuwa na mafanikio kiasi gani?

## Mwisho wa mahojiano

Asanteni sana kwa muda wako na kwa kujibu maswali yangu yote - hilo lilikuwa swali langu la mwisho kwako.

1. Je, kuna kitu kingine chochote ambacho ungependa kunishirikisha kuhusu uzoefu wako ambacho hatujakijadili?

2. Je, una swali lolote kwangu kabla hatujamaliza?

**** Mwishoni mpe RAO nakala (A3) za Matokeo na Mapendekezo (abaki nazo).***

**Maoni** - Sanduku hapa chini litajazwa na watafiti baada ya mahojiano; tafadhali andika maoni au vidokezo vyovyote muhimu ambavyo unadhani vinapaswa kushirikiwa na timu ya utafiti.

| **Maoni ya mtafiti** *(pamoja na mabadiliko)* |
|---|
| |

# Mwongozo wa usaili kwa Afisa Elimu Maalumu wa Wilaya

## Utangulizi na Idhini

**Maelekezo**: Tumia "Hati ya ridhaa ya mdomo ya mshiriki wa utafiti" ili kutoa utangulizi na kupata kibali kabla ya kuanza mahojiano. Utumie na "Idhini ya maandishi ya mshiriki wa utafiti" kupata sahihi yake"

## Taarifa za Kurekodi

*Ijazwe na mtafiti kabla ya kuanza mahojiano*

| | |
|---|---|
| **Jina la mtafiti** | |
| **Tarehe ya Mahojiano** | |
| **Maelezo ya Mshiriki** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **MKOA** | |
| **WILAYA** | |
| **Muda ambao amefanya kazi hii ya DSNEO** | miaka ______ |
| **Ana ulemavu wowote unaojulikana?** | Kama ndiyo, tafadhali onesha: ____________________ |

## Muundo wa Mahojiano

Mahojiano haya yana sehemu nne ambazo tutapitia kwa pamoja:

- Sehemu ya 1: Matokeo ya raundi ya kwanza ya utafiti
- Sehemu ya 2: Kupanga kipaumbele kwa mapendekezo ya raundi ya kwanza
- Sehemu ya 3: Mabadiliko katika MEWAKA

Majadiliano yatachunguza: Jinsi yaliyomo, muundo na njia za programu ya MEWAKA yanavyorekebishwa kulingana na muktadha tofauti (RQ1), Jinsi mahitaji mbalimbali na ushiriki sawa wa vikundi tofauti vya walimu vinavyosaidiwa katika MEWAKA (RQ2), na mafanikio na changamoto za utekelezaji wa MEWAKA kwa kiwango cha kitaifa (RQ3.)

Mjadala huu utachukua takriban dakika 45 hadi saa 1.

## Mahojiano ya Afisa Elimu Maalumu wa Wilaya

### Sehemu ya I: Utangulizi

1. Majukumu yako makuu kama Afisa wa Elimu Maalum wa Wilaya ni yapi?

   *Ikiwa wanataja wanafunzi pekee, uliza:* "Je, una jukumu lolote linalohusu walimu wenye ulemavu?"

2. Jukumu lako katika MEWAKA ni lipi?

### Sehemu ya II: Matokeo ya Utafiti ya Raundi ya Kwanza [Shughuli]

**Hatua ya 1: Eleza**: Tunataka kuwasilisha baadhi ya matokeo muhimu yanayohusiana na walimu wenye mahitaji maalum ya raundi ya kwanza ya utafiti.

**Hatua ya 2: Onesha nakala ya matokeo muhimu matatu wakati unayaeleza kwa kifupi.** [Unaweza kusitisha kurekodi ukiwa unaelezea matokeo]

<u>Matokeo:</u>

*[Angalizo: Matokeo ya utafiti wetu yamejumuishwa hapa kama mfano - yanapaswa kubadilishwa yawe matokeo ya utafiti wako]*

1. ***Walimu wenye ulemavu:*** Kati ya walimu 125 kutoka (MKOA), walimu 14 waliripoti kuwa na ulemavu uliochunguzwa kitalaamu, na 12 walikuwa na magonjwa sugu kama vile kisukari au pumu. Ni muhimu kutambua kwamba idadi ya walimu wenye ulemavu waliobainisha wenyewe ilikuwa kubwa zaidi kuliko ile iliyotolewa na walimu wakuu. Walimu wenye ulemavu waliripoti kwamba vishikwambi, moduli kutoka katika mfumo wa ujifunzaji (LMS), na programu hazina msaada wa kutosha kwa wenzao wenye uoni hafifu.

2. ***Mabadiliko***: Shule zilizo na walimu wenye ulemavu zilitumia mikakati mbalimbali ili kuongeza usawa katika ushiriki katika jumuiya za ujifunzaji, ikiwa ni pamoja na kutumia mbinu za ushirikiano na uchangamani (kama vile mijadala), kusaidia walimu wenye ulemavu kushiriki, na kuhakikisha mawasiliano yanakuwa wazi. Hakuna marekebisho ya matini za ujifunzaji zilizobainishwa. Pia wadau walibaini kutokuwepo kwa mwongozo wa namna ya kutoa msaada kwa walimu wenye ulemavu.

3. ***Mahitaji ya walimu ambayo hayawezi kutatuliwa katika ngazi ya shule kwa kiasi kikubwa yanabaki bila msaada***. Kwa mfano, mahitaji ya miundombinu ya mawasiliano, pamoja na ukosefu wa vifaa, ujuzi mdogo wa kidijitali wa walimu, upatikanaji wa vifaa vya teknolojia saidizi kwa walimu wenye ulemavu, gharama za data, kukosekana kwa mtandao, na matatizo ya upatikanaji na matumizi ya LMS.

**Hatua ya 3: Uliza maswali**

***[Anza tena kurekodi]***

1. **Uliza**: Je, kuna maswali yoyote ya ufafanuzi wa matokeo haya?
2. Nini imekugusa zaidi kutoka kwenye matokeo haya, na kwa nini?
    a. Dodosa:
        i. Nini kimekushangaza zaidi kutoka kwenye matokeo haya, na kwa nini?
        ii. Je, kuna tokeo ambalo hukutarajia kusikia, kutokana na uzoefu wako
3. Ni aina gani ya mabadiliko au msaada unayoamini ingeweza kutimiza vyema mahitaji ya walimu wenye ulemavu katika wilaya yako?
4. Ni sababu zipi zinazoweza kusababisha tofauti ya idadi ya walimu wenye ulemavu walioripotiwa na wakuu wa shule na walioripotiwa na walimu wenyewe?
5. Shule zinaweza vipi kusaidia zaidi walimu wenye ulemavu ili washiriki kwa usawa katika shughuli za JzK/MEWAKA?

## Sehemu ya III. Shughuli ya Kupanga Mapendekezo ya Raundi ya Kwanza kwa Kipaumbele

[Dakika 20]
***[Sitisha kurekodi hadi hatua ya 3]***

**Hatua ya 1: Eleza**: Kuna mapendekezo kadhaa kulingana na matokeo ya raundi ya kwanza. **Zungumzia mapendekezo yafuatayo kwa kifupi**, huku ukionesha **kadi** za mapendekezo.

Mapendekezo:

*[Angalizo: Mapendekezo ya utafiti wetu yamejumuishwa hapa kama mfano - yanapaswa kubadilishwa na mapendekezo ya utafiti wako]*

1. **Kutekeleza taratibu saidizi.** Tengeneza taratibu saidizi inayofaa kuwasaidia walimu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika shughuli za shule, ikiwa ni pamoja na mikutano ya kila wiki ya JzK na vipindi vya kila mwezi katika TRC.
2. **Kupanua dhana na ubainishaji wa ulemavu** ili kuhakikisha kwamba **takwimu** za elimu zinakusanywa kwa **usahihi**. Hii ikijumuisha taarifa za walimu wenye ulemavu wa kuona, kusikia, na kutembea, na pia kuhusisha ulemavu wa aina nyingine, kwa mfano ulemavu wa akili.
3. **Kurasimisha utoaji wa msaada kwa walimu wenye ulemavu** ili walimu hao waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za MEWAKA kwa kuandaa mwongozo toshelevu na jumuishi unaoshughulikia mahitaji na changamoto zao.
    a. Kutoa na kusaidia matumizi ya **teknolojia saidizi** kama vifaa vya usomaji wa skrini.
    b. **Kuandaa ruzuku** za wenye ulemavu ili kusaidia usafiri.
    c. **Kuanzisha mitandao ya walimu wenye ulemavu** kati ya shule na shule.

**Hatua ya 2:** Mwambie DSNEO apange kadi za mapendekezo kutokana na kipaumbele wake, yaani mapendekezo ya muhimu zaidi katika kuboresha ushiriki wa walimu wenye ulemavu katika MEWAKA/JzK. Anatakiwa kuyaweka mapendekezo katika mpangilio wa kipaumbele cha kwanza hadi mwisho. [1 ikiwa kipaumbele cha juu zaidi au muhimu zaidi hadi 6 ikiwa kipaumbele cha chini zaidi]

**Hatua ya 3:** Baada ya DSNEO kupanga kadi katika mpangilio wa kipaumbele (1 ikiwa ni kipaumbele cha juu zaidi/cha muhimu zaidi), **Anza kurekodi tena na uliza:**

1. Kwa nini X [soma kadi ya kipaumbele cha #1] ndiyo mapendekezo muhimu zaidi?

2. Je, kulikuwa na mapendekezo ambayo yalikuwa na shida katika kuyapanga kwa sababu yalionekana kuwa na muhimu sawa? Ikiwa ndiyo, tafadhali eleza kwa kifupi kwa nini.
3. Mapendekezo yetu yalipendekeza hatua kama kutoa teknolojia saidizi, ruzuku ya ulemavu, na kuanzisha mitandao ya walimu wenye ulemavu. Unafikiri nini kuhusu mawazo haya?
    a. Je, kutakuwa na changamoto yoyote katika utekelezaji wake?
4. Je, una mapendekezo mengine yoyote unayoweza kutoa kwa wilaya, mikoa au serikali kwa ajili ya walimu wenye ulemavu kushiriki katika JzK/MEWAKA kikamilifu?

*[Dokezo: Kabla ya kupiga picha ya kadi, zipe namba kwa mpangilio wa kipaumbele cha DSNEO, ukitumia kalamu rashasha inayofutika]*

**NB:** Weka kidakuzi chenye "DSNEO" tarehe na mkoa karibu na mpangilio wa kadi, kisha piga picha za kadi za mapendekezo zilizopangwa. Hifadhi picha hiyo na hakikisha inaingizwa katika transcript

## Sehemu ya IV: Mabadiliko katika MEWAKA

1. Je, unafahamu mabadiliko yoyote katika utekelezaji wa MEWAKA ngazi ya shule, yanayolenga kuhakikisha kuna ushiriki sawa wa walimu wenye ulemavu? (kama vile mabadiliko katika miundo au ratiba za vipindi vya JzK)
    a. Ikiwa ndiyo, tafadhali eleza.
    b. Umepataje taarifa kuhusu tofauti hizi au mabadiliko hayo?
        i. Dodosa: je, inaripotiwa rasmi - kwenye mikutano au ripoti zilizoandikwa? Ni ufuatiliaji wako mwenyewe kwa kutembelea/kuzungumza na shule tofauti? n.k.)
    c. Kwa maoni yako, katika utekelezaji wa MEWAKA ni mambo gani yanaweza kutofautiana kati ya shule moja na nyingine katika utekelezaji wake? [mfano: unyumbufu (flexibility) katika ratiba [scheduling] za JzK]
    d. Ni vitu gani vinahitaji kubaki sawa katika shule zote ili kuhakikisha ushiriki sawa wa walimu wenye ulemavu?
2. Kuna walimu wenye aina mbalimbali za ulemavu. MEWAKA ina msaada gani katika kukidhi mahitaji mbalimbali ya walimu hawa na kuhakikisha ushiriki wa usawa katika wilaya yako? Tafadhali toa mifano.

3. Mara nyingi inasemekana kwamba walimu wa kike wenye ulemavu hukumbana na changamoto zaidi kuliko walimu wa kiume wenye ulemavu, kwa sababu wengine wana ushirikiano mdogo na walimu wa kike wenye ulemavu. Je, umewahi kuona tofauti kama hiyo?
4. Je, ni mabadiliko gani ungependa kufanya katika MEWAKA ili kuhakikisha ushiriki sawa wa walimu wenye ulemavu?
    a. Kwa nini unadhani mabadiliko haya yataweza kuleta athari chanya?
5. Je, unaweza kuelezea jinsi walimu wenye ulemavu katika wilaya yako wanavyotumia teknolojia ndani ya MEWAKA/JzK?
    a. *Dodosa kuhusu* matumizi ya LMS, vishikwambi vya sensa kwa walimu wenye ulemavu.
    b. Je, umeshuhudia mafanikio au changamoto gani katika matumizi ya teknolojia katika MEWAKA kwa walimu wenye ulemavu?
    c. Je, kuna teknolojia saidizi zinazoweza kuwasaidia walimu wenye ulemavu kushiriki katika MEWAKA kwa urahisi zaidi?

    IKIWA NDIYO:

    d. Je, una ujuzi gani kuhusu aina mbalimbali za teknolojia saidizi zinazopatikana?
    e. Je, umewahi kuona aina yoyote ya teknolojia saidizi ikitumika?
    f. Ni aina gani ya mafunzo ambayo walimu wanahitaji ili kutumia teknolojia hiyo kwa ufanisi?
    g. Nani anapaswa kutoa teknolojia hiyo? Nani anaweza kuifanyia matengenezo?

## Mwisho wa mahojiano

Asante kwa muda wako na kwa kujibu maswali yangu yote - hilo lilikuwa swali langu la mwisho kwako.

1. Je, kuna kitu kingine chochote ambacho ungependa kuniambia kuhusu uzoefu wako ambacho hatujakijadili?
2. Je, una swali lolote kwangu kabla hatujamaliza?

Maoni — kisanduku kilicho hapa chini kitajazwa na wadadisi kufuatia uchunguzi uliofanywa, tafadhali andika tafakuri au madokezo yoyote ambayo unafikiri ni muhimu kushirikishwa kwa [TAASISI HUSIKA] au washirika wengine.

| **Maoni ya mtafiti** *(pamoja na* mabadiliko *yoyote yaliyofanywa):* |
| --- |
| |

# Mwongozo wa usaili kwa Afisa Elimu Kata (WEO)

## Utangulizi na Idhini

Maelekezo: Tumia "Hati ya ridhaa ya mdomo ya mshiriki wa utafiti" ili kutoa utangulizi na kupata kibali kabla ya kuanza mahojiano.

## Taarifa za kurekodi

*Ijazwe na mtafiti kabla ya kuanza mahojiano*

| | |
|---|---|
| **Jina la mtafiti** | |
| **Tarehe ya Mahojiano** | |
| **Mkoa** | |
| **Wilaya** | |
| **Kata** | |
| **Taarifa za mshiriki** | |
| **Jina** | |
| **Jinsi** | |
| **Jukumu** | WEO |
| **Muda ambao amefanya kazi hii [this role]** | |
| **Ulemavu wowote unaojulikana?** | Kama ndiyo, tafadhali onesha: ______________________ |

## Muundo wa Mahojiano

Mahojiano haya yana sehemu nne ambazo tutapitia kwa pamoja:

- Sehemu ya 1: Matokeo ya raundi ya kwanza
- Sehemu ya 2: Kuyapa kipaumbele mapendekezo ya raundi ya kwanza
- Sehemu ya 3: Mabadiliko katika MEWAKA

Katika sehemu ya kwanza, nitawasilisha matokeo ya Raundi ya kwanza na kisha nitakuuliza maswali, na katika sehemu zinazofuata tutafanya shughuli.

Majadiliano yetu yatachunguza muundo na mpango wa MEWAKA na jinsi inavyobadilika kuendana na mahitaji ya sehemu husika (RQ1), tofauti za walimu katika shule zenu na jinsi mahitaji yao yanavyotimizwa (RQ2), na mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa MEWAKA kwa kiwango cha kitaifa (RQ3)

Mjadala huu utachukua takriban dakika 45 hadi saa 1.

## Mahojiano ya Afisa Elimu Kata

### Sehemu ya 1: Matokeo ya Raundi ya Kwanza

**Hatua ya 1: Eleza**: Kwanza, ninapenda kuwasilisha matokeo muhimu ya raundi ya kwanza ya utafiti na kuyajadili na wewe. **[Onesha bango dogo la matokeo.]**

***1b:*** *Eleza kwamba matokeo na mapendekezo yamewasilishwa ngazi ya kitaifa (WIZARA), na tunawasilisha kwa ngazi za kata, wilaya na mkoa pamoja na shuleni**.***

**Hatua ya 2: Soma matokeo kwa kifupi** huku mshiriki akitazama matokeo yaliyochapishwa kwenye bango ndogo.

<u>Matokeo:</u>

*[Angalizo: Matokeo ya utafiti wetu yamejumuishwa hapa kama mfano - yanapaswa kubadilishwa yawe matokeo ya utafiti wako]*

1. ***Walimu wenye ulemavu:*** Kati ya walimu 125 waliojibu dodoso kutoka (MKOA), walimu 14 waliripoti kuwa na ulemavu uliochunguzwa kitalaamu, na 12 walikuwa na magonjwa sugu kama vile kisukari au pumu. Ni muhimu kutambua kwamba idadi ya walimu wenye ulemavu waliobainisha wenyewe ilikuwa kubwa zaidi kuliko ile iliyotolewa na walimu wakuu. Walimu wenye ulemavu waliripoti kwamba vishikwambi, moduli kutoka katika mfumo wa ujifunzaji (LMS), na programu hazina msaada wa kutosha kwa wenzao wenye uoni hafifu.

2. ***Mabadiliko:*** Shule zilizo na walimu wenye ulemavu zilitumia mikakati mbalimbali ili kuongeza usawa katika ushiriki katika jumuiya za ujifunzaji, ikiwa ni pamoja na kutumia mbinu za ushirikiano na uchangamani (kama vile mijadala), kusaidia walimu wenye ulemavu kushiriki, na kuhakikisha mawasiliano yanakuwa wazi. Hakuna marekebisho ya matini za ujifunzaji zilizobainishwa. Pia wadau walibaini kutokuwepo kwa mwongozo wa namna ya kutoa msaada kwa walimu wenye ulemavu.

3. ***Ushiriki wenye usawa wa kijinsia katika JzK:*** Ni asilimia 38 tu ya wawezeshaji rika walikuwa wanawake. Walimu wa kiume na wa kike hushiriki kwa usawa katika vikao vingi (8 kati ya 12) vya JzK. Aidha, katika shule 4 kati ya 12, kulikuwa na ukosefu wa ushiriki sawa. Vizuizi vinavyohusiana na jinsia vilivyobainishwa ni pamoja na umakini mdogo wa wawezeshaji rika katika kuhakikisha walimu wote wanashiriki kwa usawa. Katika JzK zilizokosa ushiriki kwa usawa, mara nyingi ushiriki wa walimu wa kike ulikuwa mdogo hasa katika vipindi vinavyohusiana na teknolojia.

4. ***Uwezo wa kukidhi mahitaji ya walimu:*** Walimu wanakidhi mahitaji yao kupitia njia zifuatazo: i) kuweka vipaumbele vya JzK, ii) kutumia data za simu za mkononi katika MEWAKA, na iii) kutoa msaada wa kiteknolojia kwa wenzao. Baadhi ya shule zilitoa vifurushi vya intaneti au chakula kwa walimu. Pia Mthibiti Ubora wa Wilaya moja alianzisha kundi la WhatsApp la walimu. Hata hivyo, karibu washiriki wote waliona kuwa walimu wana nafasi ndogo ya kufanya maamuzi, na shule kadhaa zilihisi kuwa hazikuwa na msaada ikiwa mahitaji ya kiufundishaji ya walimu yasingeweza kutatuliwa ndani ya shule.

5. ***Taratibu zinazoruhusu mrejesho ili kukidhi mahitaji ya walimu:*** Taratibu zimewekwa ili kubadilisha shughuli za JzK ili kukidhi mahitaji ya walimu ndani ya shule na kata, ikiwa ni pamoja na kushughulikia changamoto na kueneza ubunifu. Hata hivyo, mkoa wa (MKOA) pekee ndiyo uliokuwa na utaratibu wa kutoa mrejesho na kuufanyia kazi kikamilifu kuanzia ngazi ya shule, kata, Kituo cha Walimu (TRC) na wilaya.

6. ***Mahitaji ya walimu ambayo hayawezi kutatuliwa katika ngazi ya shule kwa kiasi kikubwa yanabaki bila msaada.*** Kwa mfano, mahitaji ya miundombinu ya mawasiliano, pamoja na ukosefu wa vifaa, ujuzi mdogo wa kidijitali wa walimu, upatikanaji wa vifaa vya teknolojia saidizi kwa walimu wenye ulemavu, gharama za data, kukosekana kwa mtandao, na matatizo ya upatikanaji na matumizi ya LMS.

**Hatua ya 3: Uliza maswali**

1. Je, kuna maswali yoyote ya ufafanuzi kuhusu matokeo niliyowasilisha?

2. Ni mawazo gani ya kwanza yalikujia baada ya kusikia matokeo haya?

3. Nini kimekugusa zaidi kutoka kwenye matokeo haya?
   Dodosa:
   a. Nini kimekushangaza au kukuvutia zaidi ?
   b. Je kulikuwa na tokeo ambalo hukutegemea kusikia kutokana na uzoefu wako ?

4. Je, kuna jambo lolote kutoka kwenye raundi ya kwanza ya ukusanyaji wa data ambayo unahisi hayajagusiwa vya kutosha katika matokeo yaliyowasilishwa?

5. Unapataje taarifa kutoka katika shule zako kuhusu mahitaji ya walimu ambayo yanahitaji kushughulikiwa katika mikutano ya JzK kwenye Vituo vya Walimu yaani TRC?

6. Mada za JzK zinazofanyika katika Vituo vya Walimu, klasta au kata zinapatikanaje?

7. Je, kumekuwa na mabadiliko yoyote katika utekelezaji wa MEWAKA tangu mwezi Machi ambayo ungependa kuyataja?
    a. Dodosa, kwa mfano, mabadiliko katika:
        i. Utekelezaji wa JzK kwenye vituo vya walimu?
        ii. Utendaji wa walimu katika madarasa yao?
        iii. Upatikanaji wa LMS kwa walimu?
        iv. Matumizi ya walimu ya moduli za JzK?
        v. Matumizi ya teknolojia?

8. Je, unadhani walimu wenye ulemavu bado wanakabiliwa na changamoto katika kutumia teknolojia katika MEWAKA kwenye kata yako?
    a. Ikiwa ndiyo, ni changamoto gani walimu hawa wanakutana nazo katika kushiriki katika JzK/MEWAKA?
    b. Ni mifumo gani ya utoaji msaada unatoa kwa walimu hawa ili kuhakikisha wanatumia teknolojia kwa ufanisi?
    c. Ni mabadiliko gani unayopendekeza ili walimu hawa waweze kutumia teknolojia kwa ufanisi?

9. Je, unadhani walimu wenye magonjwa sugu wanakabiliwa na changamoto katika kushiriki katika shughuli za JzK/MEWAKA katika kata yako?
    a. Ikiwa ndiyo, ni changamoto gani walimu hawa wanakutana nazo katika kushiriki MEWAKA/JzK?
    b. Ni msaada unaotoa kwa walimu hao kuhakikisha wanatumia teknolojia kwa ufanisi?
    c. Ni mabadiliko gani yanayohitajika ili kuwasaidia walimu hawa kushiriki kikamilifu na kwa usawa katika shughuli za JzK/MEWAKA?

## Sehemu ya II. Kuweka Vipaumbele kwa Mapendekezo ya Raundi ya Kwanza [Dakika 15]

**[Sitisha kurekodi hadi hatua ya 4]**

**Hatua ya 1:** Eleza kwamba kulikuwa na mapendekezo kadhaa kulingana na matokeo ya raundi ya Kwanza ya utafiti. **Onesha** nakala ya mapendekezo (A3).

**Hatua ya 2: Zungumzia** kwa kifupi mapendekezo hayo.
**Uliza**: Je, kuna maswali yoyote ya ufafanuzi wa mapendekezo haya?

Mapendekezo:

*[Angalizo: Mapendekezo ya utafiti wetu yamejumuishwa hapa kama mfano - yanapaswa kubadilishwa  na mapendekezo ya utafiti wako]*

**Taratibu Saidizi:**

1. ***Kuongeza ufahamu wa moduli za JzK:*** Hakikisha kwamba wadau wote (wakuu wa shule, wawezeshaji rika, WEOs, na DSQAOs, n.k.) wanaelewa asili ya muktadha wa MEWAKA na wana vifaa vya kutosha kusaidia na kutekeleza MEWAKA katika ngazi ya shule.

2. ***Kukuza na kutekeleza taratibu za kutoa mrejesho wa mahitaji ya walimu:*** Kushughulikia mahitaji ya walimu ambayo hayajatatuliwa katika ngazi ya shule na kuwawezesha kusambaza maarifa  na kuiga ubunifu katika MEWAKA kati ya shule moja na nyingine. Hii inaweza kujumuisha:
   a. Kuwa na mifumo bora ya kusaidia shule/walimu wanapokutana na changamoto katika utekelezaji wa JzK/MEWAKA.
   b. Kuhakikisha usambazaji endelevu wa bunifu zenye ufanisi katika ya shule zote.

**Miundombinu na Teknolojia:**

3. Kuongeza upatikanaji wa moduli za JZK kwa shule zenye mtandao za intaneti ambazo ni hafifu kwa kutathmini na kujaribisha utekelezaji wa upatikanaji wa moduli bila kutumia mtandao (offline) na/au kutafuta upatikanaji wa bure wa LMS kwa walimu kupitia watoa huduma wa mitandao ya simu.

4. Kutekeleza upatikanaji wa umeme wa jua kwa shule zisizo na umeme ili kuwawezesha walimu kuzifikia LMS na moduli za JzK.

5. Kukuza tabia za kuazimana vifaa vya teknolojia baina ya walimu katika ngazi ya  shule.

6. Kuchambua changamoto zinazojitokeza katika matumizi ya vishikwambi vilivyotolewa hivi karibuni kwa walimu katika muktadha mbalimbali wa shule.

**Usawa: Walimu wenye Ulemavu**

7. Kupanua dhana na ubainishaji wa ulemavu ili kuhakikisha kwamba takwimu za elimu zinakusanywa kwa usahihi.  Hii ikijumuisha taarifa za walimu wenye ulemavu wa kuona, kusikia, na kutembea, na pia kuhusisha ulemavu wa aina nyingine, kwa mfano ulemavu wa akili.

8. Kurasimisha utoaji wa msaada kwa walimu wenye ulemavu ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za MEWAKA kwa kuandaa mwongozo toshelevu na jumuishi utakaoshughulikia mahitaji yao na changamoto zao maalumu. Pia kutoa teknolojia saidizi kama za usomaji wa skrini, kuandaa ruzuku za walemavu ili kusaidia usafiri, na kuanzisha mitandao ya walimu wenye ulemavu kati ya shule na shule.

**Usawa: Jinsia**

9. Kuweka mikakati ya kuongeza ushiriki wa walimu wa kike katika vikao na shughuli za JzK. Hii inaweza kujumuisha:
    a. Kuteua Maafisa wa TEHAMA wa Wilaya na mabingwa wa TEHAMA wa shule kuwa na jukumu la kusaidia walimu wenye ujuzi mdogo wa kidijitali kutumia LMS na vishikwambi vilivyotolewa na serikali.
    b. Kuwepo mwongozo na ufuatiliaji ili kuhakikisha idadi ya wawezeshaji rika wa kike na wa kiume inalingana.
    c. Kuandaa warsha na mafunzo maalum ili kuwasilisha na kushughulikia matokeo kuhusu ushiriki wa jinsia na utofauti uliopo.

**Hatua ya 3: Onesha kadi zenye mapendekezo na mwambie WEO kupanga** mapendekezo kutokana na umuhimu au kipaumbele yake - yapi ni muhimu zaidi na yanapaswa kushughulikiwa kwanza, ili kuendelea kuboresha MEWAKA. [1 ikiwa kipaumbele cha juu zaidi au muhimu zaidi hadi 9 ikiwa kipaumbele cha chini zaidi]

**Hatua ya 4: Baada ya WEO kupanga kadi kwa mpangilio wa kipaumbele, Anza kurekodi tena na uliza:**

1. Kwa nini X [soma kadi ya kipaumbele cha #1] ni pendekezo muhimu zaidi?
2. Je, kulikuwa na mapendekezo yoyote ambayo yalikupa shida katika kupanga vipaumbele? Kama ndio, eleza kwa kifupi).
3. Mapendekezo yetu yalipendekeza hatua kama kutoa teknolojia saidizi, ruzuku ya ulemavu, na kuanzisha mitandao ya walimu wenye ulemavu. Unafikiri nini kuhusu mawazo haya?
    a. Je, kutakuwa na changamoto yoyote katika utekelezaji wake?
4. Je, kuna mapendekezo ya ziada unayoweza kuyatoa kwa ajili ya walimu hawa au kwa ujumla kutatua mahitaji ya walimu?

***[TIP: Before taking a photo of the cards, number them in the WEO's priority order, using a white board marker.]***

***NB:*** *Weka kidakuzi chenye "WEO" tarehe na mkoa karibu na mpangilio wa kadi, kisha piga picha za kadi za mapendekezo zilizopangwa. Hifadhi picha hiyo na hakikisha inaingizwa katika maandiko ya kikundi lengwa. [Pictures can be taken now or at the end of the interview].*

## Sehemu ya III. Mabadiliko katika utendaji wa walimu [Dakika 10]

**Hatua ya 1: Eleza:** Tungependa kujua ni mabadiliko gani walimu wamefanya kutokana na ushiriki wao katika JzK/MEWAKA.

**Hatua ya 2: Uliza maswali:**

- Kumekuwa na mabadiliko yoyote katika utendaji wa walimu kama matokeo ya moja kwa moja ya MEWAKA?

  ***Ikiwa hakuna mabadiliko yanayoonekana, ruka mpaka mwisho wa mahojiano.***

  ***Ikiwa WEO anasema, ndiyo kumekuwa na mabadiliko, uliza maswali yanayofuata*** *ili kuelewa mabadiliko vizuri zaidi.*

5. Naomba unipe mifano 3-4 ya mabadiliko ambayo umeyaona katika utendaji wa kazi au haswa katika ufundishaji wa walimu katika kata yako.
   - **Sisitiza** kwamba mifano inapaswa kuwa mahususi iwezekanavyo. Yaani, badala ya kusema "Walimu sasa wanatumia vitendo vya ushirikishwaji," WEO anapaswa kutaja ni mbinu gani walimu walianza kutumia na wametumia katika darasa na masomo gani?

     Mifano mahsusi:

     - Walimu sasa wanatumia kazi za vikundi katika vipindi vya hisabati angalau mara moja kwa wiki" au
     - "Walimu wanatumia tiketi za kutoka (exit tickets) ili kuangalia uelewa wa wanafunzi wao mara kwa mara" au
     - "Walimu walitambua mahitaji maalum ya wanafunzi wao mwanzoni mwa mwaka huu, na wanaonesha umakini wa ziada kwa wale wanaohitaji muda zaidi wa kujifunza."

## Mwisho wa mahojiano

Asante kwa muda wako na kwa kujibu maswali yangu yote - hilo lilikuwa swali langu la mwisho.

1. Je, kuna kitu kingine chochote ambacho ungependa kuongeza kuhusu ambacho hatujakijadili?
2. Je, una swali lolote kwangu kabla hatujamaliza?

*** Mpatie WEO nakala ya Matokeo na ya Mapendekezo (za A3) abaki nazo.**

Maoni — kisanduku hapa chini kitajazwa na watafiti baada ya mahojiano, tafadhali andika tafakuri au madokezo yoyote ambayo unafikiri ni muhimu.

| |
|---|
| **Maoni ya mtafiti:** *(pamoja na* mabadiliko *yoyote yaliyofanywa):* |

# Kiambatisho

## Hati ya ridhaa ya mdomo ya mshiriki wa utafiti

*[Kwa mahojiano na wawakilishi wa serikali, maafisa wa LGA, wawezeshaji kitaifa, Waratibu wa TRC]*

Hujambo, jina langu ni ____________________, na ninafanya kazi katika shirika linaloitwa_________________________________.

Awali ya yote, asante sana kwa kushiriki katika utafiti wetu. Maarifa yako yatakuwa muhimu sana kwa utafiti wetu na kuboresha utekelezaji wa _______________________ nchini ____________________. Nikupe maelezo zaidi kuhusu utafiti na kile kinachohitajika kutoka kwako, kisha unaweza kunijulisha ikiwa ungependa kushiriki au kutoshiriki.

Utafiti huu unalenga kuchunguza ___________________________. Mpango wa utafiti utaanza __________________________ hadi __________________________. Utafiti huu unafadhiliwa na______________________________________________

Tungependa kuchukua kutokana na ujuzi na uzoefu wako wa kitaalamu ili kutathmini maendeleo ya MEWAKA na jinsi inavyorekebishwa ili kukidhi mahitaji ya mwalimu kwa usawa. Tungependa kuuliza baadhi ya maswali kuhusu wewe, ushiriki wako katika kazi hiyo, na mawazo yako kuhusiana na ufanisi wa shughuli za maendeleo ya kitaaluma ya walimu ambazo zimefanyika nchini Tanzania/mkoa/wilaya/kata yako. Tunalenga kuelewa jinsi walimu wanavyojihusisha na maendeleo ya kitaaluma ya walimu (MEWAKA), na ni njia gani MEWAKA inaweza kuwa na ufanisi zaidi, usawa na kubadilika kulingana na mahitaji ya walimu na shule. Matokeo yataufahamisha mfumo wa kitaifa wa maendeleo ya walimu nchini Tanzania.

Ukichagua kushiriki, maelezo binafsi unayoniambia hayatashirikishwa kwa mtu mwingine yeyote na hayataathiri majukumu yako. Ni chaguo lako kushiriki au kutoshiriki. Ukichagua kushiriki, unaweza kukataa kujibu maswali yoyote ambayo huutajisikia vizuri kuyajibu/hautapenda kuyajibu, na unaweza kuamua kuondoka kwenye mahojiano wakati wowote. Tutafanya rekodi ya mazungumzo haya na kuitumia kuandika maelezo ya kina ya majibu ili kuyatumia katika utafiti wetu, lakini hatutakutaja kwa jina au kushirikisha maelezo yako binafsi kwa mtu yeyote nje ya timu yetu ya utafiti. Rekodi ya sauti itahifadhiwa kwa usalama na hatutaishirikisha rekodi nje ya timu ya watafiti, ambayo ni ya watafiti wa [TAASISI]. Hata hivyo, ikiwa ninaamini kuwa wewe au mtoto huenda mko hatarini, ni wajibu wangu kuripoti hili.

Data/taarifa isiyokuwa na utambulisho wako (anonymised data) inaweza kuonekana katika machapisho na mawasilisho; itatumika tu kwa madhumuni ya utafiti na maendeleo ya kitaaluma ya walimu.

1. Je, una maswali yoyote kabla hatujaanza?
2. Je, unakubali kushiriki katika mahojiano haya? [Hakikisha kila mshiriki ana nafasi ya kujibu hili]
    a. Ndio
    b. Hapana (waambie wako huru kwenda).

## Kuondolewa kwa Idhini

Idhini inayoendelea na ya hiari inaombwa kutoka kwa washiriki wote wa utafiti. Idhini ya utafiti na watoto na watu wazima walio katika hatari itatathminiwa kwa kila kesi na watoto na watu wazima walio hatarini wanapaswa kuombwa ushauri ili kupata idhini inapobidi. Washiriki wanaweza kuondoa idhini yao katika hatua yoyote ya utafiti.

Iwapo mshiriki wa utafiti angependa kuondoa idhini yake katika hatua yoyote ya utafiti, tafadhali wasiliana na [JINA, ANUANI/BARUA PEPE] au [SIMU], akionyesha sababu za kuondolewa kwa idhini. Kumbuka: hii ni ya hiari kabisa na washiriki hawatakiwi kutoa sababu ya kuondoa idhini yao. Hata hivyo, ikiwa uondoaji unahusishwa na kazi ya timu ya utafiti kwa njia yoyote ile, itakuwa taarifa muhimu ambayo itawezesha timu kujifunza na kuboresha kazi.